# Nipashe

Ijumaa Machi 27, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580190

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## CAG abaini wafu kulipwa mishahara Jeshi la Polisi

UKURASA 3




UKURASA 13

TISHIO CORONA

# Waziri amkosoa Makonda taarifa mgonjwa corona

**ASEMA** 'amesigina' kanuni za kitabibu, wagonjwa sasa wafikia 13, Mbowe ajiweka karantini, SADC yataja mikakati 12 ...*Endelea ukurasa 2, 4, 8*



Mtumishi wa Manispaa ya Kinondoni, akitumia gari kunyunyiza dawa maalum ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona katika Barabara ya Kawawa, eneo la Magomeni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## BAA LA CORONA

ZAIDI ya wafungwa 4,000 wameachiwa huru Ethiopia ikiwa ni sehemu ya mikakati ya serikali kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona huku nchi hiyo ikithibitisha kuwa na wagonjwa 12. Chukua tahadhari!

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana na kushika mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## MASHINJI, MWAMBE WAACHIWA HURU

UKURASA 3

## ...Magufuli: Uchaguzi lazima ufanyike

UKURASA 2








MICHEZO **MKUDE, CHAMA WATAJWA VIUNGO BORA** UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

## Magufuli asema uchaguzi utafanyika

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amesema licha ya kuwapo kwa tishio la homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba mwaka huu, hautaahirishwa.

Alitoa kauli hiyo jana Ikulu, Chamwino mkoani baada ya kupokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2018/19 na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Katika mkutano huo, Rais Magufuli aligusia mlipuko wa virusi vya corona, akisema si vikao vyote vilivyozuiwa na serikali kutokana na ugonjwa huo na kusisitiza kuwa wanaendelea kukutana kama walivyofanya jana.

"Vikao havijazuiwa kwa mikutano hii ya kawaida, hata Bunge ndiyo maana linaendelea, hata kwenye nchi ambazo zimeathirika kabisa zimeua mamilioni, bado mabunge yao hayajafungwa, mabaraza yao ya madiwani yanaendelea kufanya kazi.

"Kazi lazima iendelee kufanyika na uchaguzi tutafanya tu, wapo wengine wanafikiri nitaahirisha, nani anataka akae kwenye maofisi haya muda wote huo?" alihoji.

Kuhusu ripoti hizo, Rais Magufuli alipongeza Takukuru kwa kazi nzuri kisha akatangaza kumpandisha cheo Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo kuwa Mkurugenzi Mkuu.

"Hutakiwi kuwa kaimu, unatakiwa kuwa moja kwa moja kwa sababu umeweza kurudisha Sh. bilioni 8.8, utarudisha mabilioni mengine ambayo yamedhulumiwa kwa Watanzania," alisema.

Rais Magufuli alifafanua kuwa baada ya kutoa maagizo kuhusu wizi uliokuwa unafanyika kwenye Vyama vya Msingi na Ushirika katika mikoa mbalimbali, taasisi hiyo imeokoa fedha za wananchi Sh. bilioni 8.8 zilizokuwa zimeibwa.

"Umetimiza wajibu wako pamoja na chombo chako na kwamba ndani ya chombo chako wapo wabaya wachache, hasa huyu wa Kinondoni na watu wake wanne, ninalijua hilo suala. Kama yupo hapa ajue, ndio ubaya wangu, nachapa hapa hapa.

"Lakini kwa kweli, taasisi hii imefanya kazi nzuri, nitoe wito kwa viongozi kuanzia mimi, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, wakuu wa mikoa hadi chini... tutimize wajibu wetu katika kudhibiti dhuluma zinazowagusa watu wadogo; wakulima, wafugaji, wavuvi, ili siku nyingine Takukuru tukiituma, ikute kazi zote zimefanywa na viongozi wa huko kwa sababu wana madaraka hayo," aliagiza.

Rais Magufuli alitaka watendaji wenzake hao wajiulize swali aliloliita dogo kwamba: "Katika maeneo hayo, hakuna viongozi waliokabidhiwa madaraka ambao wanalipwa mishahara na wakati hayo yakiendelea walikuwa wanafanya nini?"

"Kwa nini wananchi wa kawaida wamelima mazao yao hawalipwi fedha zao, viongozi wapo ofisini, wana magari na wana simu, lakini Sh. bilioni 8.8 zinaliwa na sisi tupo?

"Siku moja nilimwambia Waziri Mkuu, kwamba unatoka Lindi nimekuwa nikikusikia mahali pengine ukikemea vizuri sana, kwanini wananchi wa Lindi wadhulumiwe ufuta wa Sh. bilioni 1.2?

"Kwa nini mpaka chombo cha kushughulikia rushwa ndiyo kiende kikafanye kazi ya kuwarudishiwa wananchi fedha zao ambazo wamelima kwa nguvu zao, lakini wamedhulumiwa?" Alihoji.

Rais Magufuli alisema ripoti ya CAG ataikabidhi kwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Katibu Mkuu Kiongozi ili wayafanyie kazi maeneo yao yanayowahusu.



Rais Dk. John Magufuli akiwa ameshika taarifa ya mwaka 2018/2019 ya CAG, pamoja na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, baada ya kuwakabidhi pamoja na taarifa ya Takukuru, kwa ajili ya kuzifanyia kazi, katika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Waziri amkosoa Makonda taarifa mgonjwa corona

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA MJINI

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amekosoa utaratibu uliotumika na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kutoa taarifa kuhusu kuambukizwa virusi vya corona kwa mtoto wa Mwenyekiti wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe.

Amesema kutaja ugonjwa wa mtu ni kwenda kinyume cha taratibu za kitabibu, akiwataka wananchi kuamini taarifa za ugonjwa wa corona zinazotolewa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Waziri wa Afya na Waziri Mkuu.

Sambamba na hilo, amesema hadi sasa Tanzania imejitahidi kudhibiti maambukizo ya ndani kwa ndani ya ugonjwa huo na wasafiri 245 walioingia nchini tangu Machi 23 mwaka huu, wametengwa kwenye hoteli na maeneo yaliyoandaliwa.

Ummy aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari, ambao pamoja na mambo mengine, walihoji uhalali wa taarifa iliyotolewa na Makonda siku tatu zilizopita kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo.

Akijibu swali hilo, waziri huyo alisema kwa mujibu wa taratibu za kitabibu, ugonjwa ni siri kati ya mgonjwa na daktari.

"Suala la RC (Mkuu wa Mkoa) wa Dar es Salaam kwenye hili niseme tu kwa ufupi taratibu za kitabibu zipo wazi, ugonjwa ni siri kati ya mgonjwa na daktari, ndiyo maana kwenye taarifa zangu zote, sijawahi hata siku moja kutaja jina zaidi ya kusema mgonjwa huyu mwanamke au mwanaume na umri wake, na aliingia nchini tarehe fulani. "Sijataja jina, Isabela alitajwa na baadhi ya watu na yeye mwenyewe alijitaja, na alivyojitaja na sisi tukamtaja, MwanaFA alijitaja mwenyewe, na pia Sallam ambaye ni Meneja wa Mwanamuziki Diamond Platnums," alisema.

Ummy alisema taratibu zinazuia kutaja majina na Rais John Magufuli alishatoa maelekezo kuwa Watanzania waamini taarifa zinazotolewa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Wizara ya Afya Tanzania na Zanzibar na Waziri Mkuu.

"Sasa kama kuna mtoto wa huyu, ndiyo maana na wenyewe walijitaja, lakini mimi na naibu wangu na Katibu Mkuu hamtatusikia hata siku moja tukitaja jina la mgonjwa kwa sababu ni kinyume cha maadili, miongozo na taratibu za kitabibu nchini," alisema.

Akizungumzia mwenendo wa ugonjwa huo nchini, waziri huyo alisema wizara yake kwa kushirikiana na ya Zanzibar, imeendelea kufanya ukaguzi kwa kupima joto la mwili kwa wasafiri wote wanaoingia nchini.

"Kuanzia Januari Mosi mwaka huu hadi sasa, wasafiri 1,890,532 wamefanyiwa ukaguzi wa kupimwa joto kwenye vituo 27 vya mipakani ikiwamo viwanja vya ndege na bandarini na kwa saa 24 zilizopita, jumla ya wasafiri 3,471 wamefanyiwa 'screening'," alisema.

Alibainisha kuwa watu 273 wamepimwa sampuli za kupima virusi vya corona katika Maabara Kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii hadi jana huku Zanzibar wakiwa ni 30.

Ummy aliongeza kuwa kati ya wagonjwa hao, mmoja ndiyo hakusafiri nje ya nchi katika siku 14 zilizopita kabla ya kuthibitika kuugua na alipata maambukizo kutoka kwa mtu aliyekuwa nje ya nchi.

### MGONJWA WA KWANZA

Ummy alisema mgonjwa wa kwanza wa Arusha, Isabela, amepona corona na taratibu za kumruhusu kurudi nyumbani zinaendelea, hivyo mkoa huo utabaki na mgonjwa mmoja. "Mgonjwa wetu amepona COVID19 na amepimwa mara tatu hana, tumeanza utaratibu wa kumrudisha nyumbani, kazi ambayo nimemwelekeza Katibu Mkuu aifanye sasa hivi suala la kutoa elimu ili kuondoa unyanyapaa, kulaumiana na kunyooshewa vidole Isabela," alisema.

### 245 WATENGWA

Waziri huyo alisema wasafiri 245 walioingia Tanzania Bara na Zanzibar wamewekwa karantini kwa siku 14 kwenye maeneo maalum yaliyobainishwa na serikali kwa gharama zao. Kwa upande wake, Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, aliwataka Watanzania kujikinga na ugonjwa huo huku akisisitiza kuwa serikali haina nia ya kumweka mtu kambini kumtesa.

"Huu ugonjwa tunapaswa kujikinga, mwanangu alishukiwa na akachukuliwa kipimo kuangalia katika kumuuliza akasema amekutana na watu 50 nikiwamo na mimi. Je, tuna uwezo wa kuchunguza watu wote? Mtu atakayepata ishara, ajitokeze na kueleza watu aliokutana nao.

"Hii si kazi ndogo, kila mtu anapiga kelele, sisi Watanzania hali ilivyo tujitahidi kupeana nafasi hii inapunguza maambukizo kwa asilimia 50, tuwasikilize viongozi wetu," alisihi.

### MBOWE AJITENGA

Akizungumza akiwa kwenye eneo la kijitenga nyumbani kwake jijini Dodoma, Mbowe alisema familia imejitenga ili isiambukize wengine.

"Mimi nipo Dodoma, lakini nimeamua kujitenga, kukaa nyumbani na kufanya kazi kutoka nyumbani, nimepima, nasubiri majibu yangu, kama sijatapa, nitamshukuru Mungu, lakini kama nimepata, nitaanza matibabu.

"Mgonjwa (mwanawe) yupo eneo lake. Ndugu, marafiki kuna watu tumekutana nao tumesafiri kwenye ndege, mabasi na magari. Tangu nimeachana na mwanangu siku 12 zilizopita, nimekwenda Arusha, Moshi, Dodoma na nimehudhuria mazishi, nimekutana na watu wengi.

"Mheshimiwa Rais kanipigia simu kanipa pole, ameipa pole familia na amempa pole mtoto... nashauri serikali iunde kikosi kazi na kuwe na maeneo ya huduma za haraka kwa kuwawahi watu na kuwapa huduma za msingi, vyuo vina mabweni, yatumike watu wawekwe na kupewa huduma," alishauri.

## HABARI KITAIFA

# Mashinji, Mwambe waachiwa huru

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, imewaachia huru washtakiwa tisa wakiwamo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vincent Mashinji na aliyekuwa Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe.

Mbali na vigogo hao, wengine ni Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Zubeda Sakuru, aliyekuwa Katibu wa Chadema kanda ya Kusini, Filbert Ngatunga, aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Ruvuma, Ereneus Ngwatura na aliyekuwa katibu wa Chadema Mkoa wa Ruvuma. Delpin Gazia.

Wengine ni Charles Makunguru, aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Chadema Wilaya ya Nyasa , Diwani wa Lipingu ambaye pia ni mnadhimu wa madiwani wa Chadema Kanda ya Kusini Cuthbert Ngwata na Sang`uda Manawa ambaye ni ofisa kutoka Chadema makao makuu, Dar es Salaam.

Washtakiwa hao wameachiwa huru baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao.

Akitoa hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Cleofasi Waane, alisema mahakama imesikiliza maelezo ya upande wa mashtaka yaliyotolewa na mashahidi wanne ambao walidai kuwa washitakiwa wote kwa pamoja katika tarehe isiyofahamika walifanya njama ambazo zilisababisha wafanye kosa la kufanya mkusanyiko usio na kibali.

Hakimu Waane alisema washtakiwa hao walidaiwa kufanya hivyo katika mji mdogo wa Mbamba BBay wilayani Nyasa.

Pia walishtakiwa kwa madai kwamba Julai 15, 2017 washtakiwa wote kwa pamoja walisababisha mkusanyiko mkubwa wa watu ambao ulianza na pikipiki na magari yaliyokuwa yanapeperusha bendera za Chadema wakati wakijua kuwa kufanya hivyo ni kosa.

Alisema pamoja na maelezo hayo washtakiwa baada ya kudaiwa kufanya makosa hayo walikamatwa na kufunguliwa mashtaka ambayo kila mmoja alikana.

# CAG abaini wafu kulipwa mishahara Jeshi la Polisi

**Na Romana Mallya**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini ufujaji wa mamilioni ya shilingi ndani ya Jeshi la Polisi kupitia mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara ya Sh. milioni 193.13 kwa watumishi 11 waliofariki dunia, kufukuzwa kazi au kustaafu.

Kashfa hiyo mpya ndani ya jeshi hilo, iliibuliwa jana na CAG, Charles Kichere, alipowasilisha kwa Rais John Magufuli ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Alisema ukaguzi wake umebaini dosari nyingine katika matumizi ya fedha za umma kwenye malipo ya Sh. milioni 806.69 yaliyofanywa na jeshi hilo katika ujenzi wa majengo yake.

"Katika kupitia malipo yaliyofanyika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 400, mabweni na nyumba za madarasa, nilibaini dorasi zifuatazo; malipo ya vibarua kabla ya ununuzi wa vifaa Sh. milioni 355.2, malipo akaunti binafsi badala ya fundi mchundo aliyesaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi Dodoma Sh. milioni 45.2.

"Malipo ya zaidi kwa kulinganisha na kiwango kilichochukuliwa kwenye jedwari la mahitaji kama gharama za vibarua kwenye ujenzi wa nyumba 30 zilizopo eneo la Medeli Mashariki Dodoma ya Sh. milioni 92.64.

"Malipo kwa ajili ya vibarua ili kujenga msingi, kuta na rinta hayakuwa sehemu ya jedwali la mahitaji Sh. milioni 105. Uongozi ulilipa tofali lenye ukubwa wa inchi sita kwa Sh. 1,800, lakini mzabuni alipeleka tofali za inchi tano zinazouzwa kwa Sh. 1,300, hivyo kusababisha kulipa zaidi Sh. milioni 54.

"Bidhaa za ujenzi zilizolipwa ambazo hazikuwapo eneo la ujenzi Sh. milioni 54.65, hivyo kujengwa kwa Sh. milioni 806.69," alibainisha. Kutokana na dosari hizo, CAG Kichere aliishauri serikali kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wakati wa utekelezaji wa shughuli zote.

**DENI LA TAIFA**

CAG pia alisema deni la serikali hadi kufikia Juni 30 mwaka jana, lilikuwa Sh. trilioni 53.11. Kati yake, deni la ndani Sh. trilioni 14.86 na la nje Sh. trilioni 38.24 ikiwa ni ongezeko la Sh. trilioni 2.18 (asilimia 4) kulinganishwa na deni la Sh. trilioni 50.93 lililoripotiwa Juni 30, 2018.

Alisema ongezeko la deni limesababishwa na riba ya mikopo halisi na kushuka kwa thamani ya shilingi, lakini akasisitiza kuwa uchambuzi uliofanyika unaonyesha bado linaendelea kuhimilika.

Kiongozi huyo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, aliwasilisha kwa Rais Magufuli ripoti 19 zinazohusu masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi wa serikali kuu, ukaguzi wa mamlaka za serikali za mitaa, ukaguzi wa mashirika ya umma, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na ukaguzi wa mifumo ya Tehama.

Ripoti hizo pia zinahusisha ukaguzi wa ufanisi, ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za ukaguzi wa ufanisi kwa miaka iliyopita na ripoti 12 za ukaguzi wa ufanisi kati sekta mbalimbali. Alisema katika ukaguzi huo, ametoa hati za ukaguzi 1,082, zinazoridhisha zikiwa 1,017 (asilimia 94), zenye shaka ni 46, zisizoridhisha saba na mbaya 12.

Alizitaja taasisi ambazo zimepata hati zisizoridhisha kuwa ni Ubalozi wa Tanzania Ethiopia, Kampuni ya Stan Gold, Tume ya Taifa ya Mpango wa Utumiaji wa Bora wa Ardhi na Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Katika ukaguzi wake kwenye hesabu za vyama vya siasa, CAG Kichere alidokeza kuwa vinne vimepata hati isiyoridhisha na 11 vimepata hati mbaya.


CRDB BANK
Tunakusikiliza

TANGAZO KWA UMMA

UHAIRISHWAJI WA SEMINA KWA UMMA

Benki ya CRDB inatoa taarifa kwa umma kwamba semina zilizopangwa kufanyika nchi nzima siku ya **Jumamosi tarehe 4 Aprili 2020** zimeahirishwa mpaka itakapotangazwa tena.

Semina hizo zimeahirishwa kutokana na agizo la serikali la kusitisha mikusanyiko yote nchini ikiwa ni juhudi za kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa **COVID-19** *(Corona)*
Benki inaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

**Imetolewa na Katibu wa Benki kwa idhini ya Bodi ya Wakurugenzi.**



MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority
ISO 9001: 2015 CERTIFIED

TAARIFA KWA UMMA

24 Machi, 2020

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU HUDUMA ZITOLEWAZO NA MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA WAKATI WA TISHIO LA UGONJWA WA COVID-19

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inapenda kuwatangazia wadau wake kwamba kutokana na tishio la ugonjwa wa homa kali ya mapafu ujulikanao kwa jina la Covid-19 ambao unasababishwa na virusi vya Corona, hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Serikali pamoja na Taasisi zake kama tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa huu ambao umeingia nchini.

2. Hivyo kuanzia tarehe 25 Machi, 2020 huduma za TMDA zitatolewa kwa utaratibu ufuatao:

(a) Vibali vya uingizaji na utoaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vitatolewa kwa kupitia mfumo wa kielektroniki na kutumwa kwa waombaji moja kwa moja.

(b) Maombi ya usajili wa bidhaa yawasilishwe kwa mfumo wa kielektroniki na ufuatiliaji wake ufanywe kwa mawasiliano ya simu na barua pepe kupitia kwa Mameneja wa sehemu husika.

(c) Kwa huduma nyingine ambazo hazitolewi kwa mifumo ya kielektroniki, wateja wanaombwa wafike katika ofisi za TMDA katika maeneo mbalimbali ya nchi endapo tu kuna ulazima huo na wanashauriwa watumie zaidi mawasiliano ya simu na mitandao kupata huduma kupitia maofisa wafuatao:

| Na. | Jina la Afisa | Cheo | Na. ya simu | Barua pepe |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Emmanuel Alphonce | Meneja, Ukaguzi na Udhibiti wa Dawa na Bidhaa Nyongeza, Ofisi Ndogo TMDA, Dar es Salaam | 0754 284367 | emmanuel.nkiligi@tmda.go.tz |
| 2. | Bw. Sunday Kisoma | Meneja, Udhibiti wa Vifaa Tiba na Vitendanishi, Ofisi Ndogo TMDA, Dar es Salaam | 0713 278977 | sunday.kisoma@tmda.go.tz |
| 3. | Bw. Felchism Apolnary | Meneja, Usajili wa Dawa, Ofisi Ndogo TMDA, Dar es Salaam | 0713 477536 | felchism.apolinary@tmda.go.tz |
| 4. | Dr. Alex Nkayamba | Kaimu Meneja, Udhibiti na Majaribio ya Dawa, Ofisi Ndogo TMDA, Dar es Salaam | 0713 868890 | alex.nkayamba@tmda.go.tz |
| 5. | Bi. Sophia Ally | Kaimu Meneja, TMDA Kanda ya Ziwa, Mwanza | 0652565605 | sophia.mziray@tmda.go.tz |
| 6. | Bi. Anita Mshighati | Kaimu Meneja, TMDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya | 0687 239387 | anitha.mshighati@tmda.go.tz |
| 7. | Bw. Proches Patrick | Kaimu Meneja, TMDA Kanda ya Kaskazini, Arusha | 0714 836725 | proches.kimario@tmda.go.tz |
| 8. | Dr. Edgar Mahundi | Meneja, TMDA Kanda ya Magharibi, Tabora | 0654 817849 | edgar.mahundi@tmda.go.tz |
| 9. | Bi. Sonia Mkumbwa | Kaimu Meneja, TMDA Kanda ya Kati, Dodoma | 0715 302440 | sonia.mkumbwa@tmda.go.tz |
| 10. | Dr. Engelbert Bilashoboka | Meneja, TMDA Kanda ya Kusini, Mtwara | 0766 729416 | engelbert.mbekenga@tmda.go.tz |
| 11. | Bw. Adonis Bitegeko | Meneja, TMDA Kanda ya Mashariki, Dar es Salaam | 0655 222662 | adonis.bitegeko@tmda.go.tz |
| 12. | Bw. Ambele Mwafula | Meneja, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano | 0713 305193 | ambele.mwafula@tmda.go.tz |
| 13. | Bw. Moses Magoma | Meneja, Rasilimali Watu na Utawala | 0655 888831 | moses.magoma@tmda.go.tz |

(d) Mamlaka inawaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza katika kipindi hiki cha mpito.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba
S.L.P 1253, Dodoma Au
S.L.P 77150, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751
Barua Pepe: info@tmda.go.tz
Simu bila malipo: 0800110084

215681902

# Mawaziri Afya SADC wapitisha mambo 12



**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAWAZIRI wa Afya na Maendeleo ya Jamii katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, wamekubaliana mambo 12 ya kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona na kuruhusu usafirishaji wa bidhaa na huduma.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (pichani), alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo.

Alisema katika kikao chao walichofanya kwa njia ya mtandao (video conference) chini ya Mwenyekiti wao Dk. Daniel Ngamije, wamejadili mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema wakubaliana kuruhusu usafirishaji wa bidhaa na huduma ndani ya Afrika Mashariki na kuweka masharti mbalimbali ya kuzingatiwa.

"Tumeweka masharti kwamba watu kwenye gari moja la mizigo wasizidi watatu, kutakuwa na watu wawili hadi watatu ambao watavuka mpaka na tumekubaliana wawe kwenye afya njema na watafanyiwa screening (kuchunguzwa) na endapo watabainika wana dalili za maambukizi watazuiwa kuendelea na safari," alisema.

Alisema madereva wa magari hayo watakaobainika na maambukizi watawekwa chini ya uangalizi kwa siku 14 na kuwataka wamiliki wa magari kuandaa madereva watakaoendesha wakiwa na afya njema.

"Pia tumekubaliana kubadilishana taarifa na uzoefu kupitia vikosi kazi na tumekubaliana kila nchi itateua mtu mmoja atakayefanya kazi na sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Alisema mawaziri wameiagiza Tume ya Utafiti ya Afrika Mashariki kufanya utafiti kuhusu dawa, chanjo, wagonjwa na sera.

"Tumekubaliana kuweka chini ya uangalizi wa siku 14 kwa abiria wote wanaoingia kwenye ukanda wetu na kuepuka kuwa na maambukizi mapya," alisema.

Ummy alisema wamekubaliana kuwa na ukaguzi kwa wasafiri wanaotoka nje ya nchi badala ya kufanya kwa wanaoingia.

"Pia kuwezesha kampuni za Afrika Mashariki kwa ajili ya kuzalisha dawa, vifaa na vifaa kinga vitakavyotumika," alisema.

Makubaliano hayo alisema yamesainiwa na mawaziri kutoka nchi za Rwanda, Kenya, Burundi, Sudani Kusini, Uganda na Tanzania.

# Mahakama kutoa uamuzi hoja dhidi ya Makandage

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imesema itatoa uamuzi dhidi ya hoja za mshtakiwa wa tatu, Joseph Makandage, baada ya jana kuwasilisha kwa njia ya maandishi kwamba hati ya mashtaka ya kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili na wenzake wawili ina upungufu kisheria.

Awali Makandage aliomba kuwasilisha maombi hayo nje ya muda, lakini kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona washtakiwa hawakupelekwa mahakamani wako mahabusu.

Wakili wa utetezi, Alex Balomi, alidai kuwa hoja za mshtakiwa ziko tayari na watazi-wasilisha mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, kwa njia ya maandishi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba tarehe ya uamuzi.

Katika maombi yake, Makandage anadai hati ya mashtaka dhidi yao ina upungufu wa kisheria na anaiomba mahakama kuitupilia mbali iwaachie huru au itoe amri nyingine yoyote ambayo inaona inafaa.

Hakimu Shaidi alisema mahakama yake itatoa uamuzi Aprili 9, mwaka huu.

Machi 12, mwaka huu, upande wa Jamhuri katika kesi hiyo baada ya kupitia maombi ya mfanyabiashara James Rugemarila, uliiomba mahakama kuyatupilia mbali kwa sababu haina mamlaka ya kutoa uamuzi wake.

Pia ulidai kuwa maombi hayo yamewasilishwa wakati ambao si mwafaka.

Rugemarila aliomba kuwasilisha hoja, kuomba kuondolewa katika kesi ya uhujumu uchumi na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP).

TANGAZO


Yajayo
hayatabiriki
Pata Bima ya Maisha
inayokupa akiba kwa ajili
yako na ya wale uwapendao
Jipange
Sanlam
CRDB
INSURANCE
Tunakusikiliza

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuendelee kubuni njia za kuepukana na corona

**JANA** Waziri wa Afya, Maendelo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alieleza kuwa Tanzania ina watu 13 walioambukizwa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19).

Kati ya watu hao, Watanzania wanane na raia wa nje watano na kati yao, mmoja pekee alipata akiwa nchini, baada ya kukutana na mtu aliyetoka nje ya nchi.

Alitaja mikoa na idadi ya wagonjwa ni Arusha (2), Dar es Salaam (8), Zanzibar (2) Kagera (1) na wote walisafiri nje ya nchi katika siku 14 zilizopita kabla ya kuthibitika kuugua.

Upimaji wa COVID-19 unafanyika kwa kupima joto la mwili kama kuna homa na hadi sasa watu 1,890,532 katika vituo 27 vya mipakani, viwanja vya ndege na bandarini walipimwa tangu kuanza kwa ugonjwa huo na kwa saa 24 zilizopita hadi jana asubuhi watu 3,471 walipimwa kupitia vipimo rasmi.

Nyingine ni kupima sampuli za washukiwa wa COVID-19 katika maabara kuu ya taifa ya afya ya jamii, na hadi jana asubuhi watu 273 kati yake 243 wa Tanzania Bara na 30 wa Zanzibar.

Waziri alieleza kuwa hadi sasa hakuna maambukizi ya ndani bali wengi wametoka nje, na kwamba wa mkoani Kagera ni dereva wa malori makubwa aliyepitia mpaka wa Kabanga wa Tanzania na Burundi.

Alieleza kuwa kuna jumla ya watu 245 wamewekwa kwenye uangalizi wa kujitenga (self isolation) ambapo 134 wako Zanzibar na 111 Tanzania Bara.

Tunapongeza kazi nzuri iliyofanywa na inayoendelea kufanywa na serikali katika kupambana na corona, ambayo ni tishio duniani, na hadi sasa maelfu ya watu wamefariki wengi wakiwa ni wazee na watoto.

Kutokana na tishio hilo na taarifa za kueleza kuwa virusi hivyo vina uwezo wa kuishi kwa siku tatu kwenye eneo lolote, ndiyo maana serikali yetu imetoa maelekezo kadhaa kama njia ya kujikinga kwa kuwataka wananchi kunawa kwa maji tiba kila wakati au kunawa kwa sabuni na maji yanayotiririka.

Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na serikali, bado kuna jambo jingine, ambalo sisi Nipashe tunaliona ni muhimu kufanyika, ni kuwa na maabara zinazotembea (mobile laboratory) ili watu wengi hasa wa mikoa ya mipakani na yenye watu walioshaambukizwa kupimwa haraka zaidi na kuchukua hatua.

Kwa sasa ni mtu mmoja pekee wa nchini ambaye alikutana na mtu aliyetoka nje mwenye maambukizi, na hadi sasa, hivyo inakuwa vigumu kujua kama wote aliokutana nao wamewekwa chini ya uangalizi au aliyewakumbuka wote, na kama alishika mahali na virusi kubakia, huku ikielezwa na wataalamu kuwa vinaweza kukaa mahali kwa siku tatu.

Kwa kuwa sisi kama taifa hatunabudi kuendelea kuweka tahadhari ya kujikinga na maambukizi, tunapendekeza kuwa uanzishwe utaratibu wa kupima watu sehemu za kazi kwa kuwa itasaidia watu kufanya kazi kwa uhuru zaidi.

Utaratibu huo pia ni vizuri kuanzishwa na kutekelezwa katika maeneo yenye mwingiliano mkubwa wa watu.

Tunaamini uwapo wa maabara hizo utawezesha watu wengi kupimwa na kuchukua hatua za kujitenga kwa haraka kabla ya kuambukiza wengine.

Tunapendekeza hivyo, kutokana na hivi karibuni kuwapo raia waliotoka nje ya nchi, ambao walipelekwa katika moja ya hoteli jijini Dar es Salaam, lakini walishindwa kumudu gharama, lakini haijulikani kama walihifadhiwa kwingine au walikwenda kujitenga wenyewe. Tunaendelea kuamini na kusisitiza kuwa kwa kuwa na maabara inayotembea, watu wengi watapimwa na hofu iliyoingia kwenye jamii itapungua.

Tunaona kuwa litakuwa jambo zuri kwa Tanzania kuendelea kufuatilia mwenendo wa ugonjwa huu na kubuni njia mbadala kama hizi za kuepukana na maambukizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Enyi mnaoishi huko pembezoni, msiache fursa hizi za kifedha

**MPANGO** wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha, unalenga kuleta mabadiliko chanya katika maeneo makuu manne, kupunguza vikwazo vya ushirikishwaji wa Watanzania kwenye mfumo rasmi wa fedha wa nchi.

Maeneo hayo ni kuongeza kufikiwa huduma za fedha, kuboresha Tehama za utoaji huduma na mawasiliano kwa wateja, kuelimisha wateja na kulinda haki zao katika matumizi ya huduma mbalimbali za fedha.

Serikali inakusudia kuongeza kiwango cha wananchi kuwa karibu na huduma za kifedha, kutoka umbali usiozidi kilometa tano kutoka asilimia 86 mwaka 2017 hadi asilimia 90 mwaka 2022.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, bado kuna changamoto ya umbali wa kutoka walipo wananchi na sehemu ya kupata huduma za kifedha, hali ambayo kwa namna moja au nyingine, husababisha usumbufu kwao.

Mpango huo pia unalenga kuongeza kiwango cha wananchi wanaotumia mara kwa mara huduma za kifedha kupitia taasisi za fedha na mitandao ya simu kutoka asilimia 65 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 75 mwaka 2022.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anasema huo ni mpango wa pili wa taifa wa huduma jumuishi za kifedha wa kuwajengea wananchi mtindo wa kujiwekea akiba.

Nikirejea katika hoja ni kwamba, suala la kusogeza huduma za kifedha karibu na wananchi ni la muhimu na ndiyo maana baadhi ya benki zimefungua matawi kwenye baadhi ya vijiji nchini au kuweka mawakala.

Vilevile kuna baadhi ya vijiji ambavyo sasa taratibu zinafanyika ili kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma hiyo inayosudiwa na serikali kwamba wananchi waipate kwa umbali mfupi.

Miongoni mwa vijiji hivyo ni vya wilayani Musoma Mkoa wa Mara ambavyo, benki tatu za NMB, CRDB na NBC zimeombwa kuepeleka huduma zake ikiwa ni njia ya kusogeza huduma za kifedha karibu na wananchi na hasa hao wa pembezoni.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, taasisi hizo za fedha zimeonyesha ukubali wa kujenga matawi kwenye baadhi ya vijiji ili kuondolea wananchi kusafiri umbali mrefu.

Lakini, wakati mchakato wa kufungua matawi ukiendelea, siyo vibaya kuweka mawakala wa kutosha, ambao watatoa huduma hizo kwenye baadhi ya vijiji kuliko kusubiri hadi kujengwa majengo ya benki.

Eneo hilo linatajwa kuwa na vijiji 68, lakini inaelezwa kuwa kuna mawakala katika vijiji vya Mugango, Bukima na Murangi, hali ambayo inaonyesha wananchi wengi hawajafikiwa na huduma hiyo.

Kwa mujibu mkuu huyo wa wilaya, kuna vijiji vingine kama Suguti, Saragana, Busekela, Seka, Bwai Paris na Kigera Etuma, kwa vile vina mazingira mazuri ya kuvutia benki kuwa na mawakala.

Niseme kuwa, ni fursa nzuri kwa wananchi wa vijijini, ambayo wanapaswa kuichangamkia kwani itawasaidia kuwapunguzia kusafiri umbali mrefu, ambao kimsingi ni sawa na kupoteza muda.

Pia, suala la elimu inayohusiana na mambo ya fedha, kimsingi ni la muhimu, kwani katika malengo makuu manne ya Mpango wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha, elimu inatajwa.

Elimu hii kimsingi ni la muhimu, na inaweza kufungua fursa mpya katika wateja wapya, kama vile wateja wanaohama benki moja kwenda nyingine, hivyo hapo ndipo unapokuja umuhimu wa elimu.

Mbali na kufungua fursa mpya katika wateja wapya, elimu hii pia inaweza pia kujenga sifa nzuri, katika ngazi mbalimbali za jamii na kuimarisha uhusiano na wateja wa ndani pamoja na jamii.

Huduma za kifedha karibu na wananchi pamoja na elimu vinaweza kusaidia biashara kukua na kuziongezea taasisi hizo mapato kupitia huduma zinazotolewa.

Kimsingi ni kwamba huwezi kumkamua ng'ombe usiyemlisha, hivyo suala la elimu na hata ushauri ni vya muhimu, badala ya taasisi za fedha kuwa wakopeshaji tu kwa ajili ya biashara ndogo au kubwa, bali biashara nayo inahitaji elimu na ushauri ili iweze kuimarika.

# Uvuvi wa sumu watisha wananchi kutumia maji

**Na Happy Severine,** MASWA

WANANCHI wa mji wa Maswa, mkoani Simiyu wameiomba Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira mjini Maswa (Mauwasa), kusitisha huduma ya maji baada ya kubainika kuwapo kwa uvuvi haramu wa kutumia sumu kuvulia samaki katika bwawa la New Sola lililoko kijiji cha Zanzui, ambalo ndicho chanzo kikuu cha maji katika mji huo.

Wakizungumza jana kwa nyakati tofauti mjini Maswa, baadhi ya wananchi hao ambao ni wateja wa mamlaka hiyo walisema wameshtushwa na taarifa hizo za watu kuvua samaki katika bwawa hilo kwa kutumia dawa ya Thiodan.

Walisema kwa sasa wanahofia kuyatumia maji hayo yenye sumu ambayo huenda ikawaathiri afya zao taratibu na kuiomba mamlaka hiyo kusitisha utoaji huduma za maji kwao ambayo yanatoka katika chanzo hicho hadi uchunguzi utakapofanyika.

"Tumeona taarifa ya Mkuu wetu wa wilaya, Dk. Seif Shekalaghe, kupitia vyombo vya habari kuwa wamegundua kuna uvuvi haramu tena wa kutumia sumu kuvulia samaki katika chanzo chetu kikuu cha maji katika bwawa letu la New Sola," alisema.

"Kwa sasa tumeingiwa na hofu ya kutumia maji maana ndiyo tunayatumia kwa matumizi yetu ya nyumbani, mie niiombe Mauwasa isitishe kwanza huduma ili kujiridhisha kuwa yanafaa kwa matumizi ya binadamu," alisema Eliza Thomas.

Walisema kuwa hadi sasa wanaogopa kuyatumia maji hayo baada ya taarifa hiyo kutolewa na serikali wilayani humo, huku wakiitupia lawama mamlaka hiyo kwa kushindwa kulilinda bwawa hilo ambalo ndiyo uhai wao.

"Tunaogopa kuyatumia maji haya tangu tupate taarifa hizi, lakini changamoto tuliyonao hatuna chanzo kingine cha maji na lawama hizi za maji kuchafuliwa kwa sumu Mauwasa hawawezi kuzikwepa kwa kuwa ndiyo wenye dhamana ya kulilinda bwawa hili," alisema Zacharia Charles.

Walisema kuwa uharibifu wa mazingira katika bwawa hilo na hadi sasa kufanyika uvuvi huo ambao unahatarisha maisha yao, inatokana na jamii inayozunguka bwawa hilo kutokuwa na uhusiano mzuri na mamlaka hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Mauwasa, Mhandisi Nandi Mathias, alisema kuwa watachukua sampuli ya maji na kuituma katika maabara ya maji iliyoko mjini Shinyanga, lakini wataendelea kusukuma maji wakiamini maji ni salama.

Bwawa la New Sola linahudumia wakazi wapatao 120,000 wa mji wa Maswa na vijiji 11 vilivyoko katika wilaya hiyo.

## Bil. 35/- kutekeleza miradi ya kiuchumi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Shinyanga inatarajia kutumia Sh. bilioni 35 kutoka ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu mikubwa ya maendeleo ambayo itachochea ukuaji wa uchumi.

Hayo yalibainishwa jana na Mtakwimu wa Manispaa ya Shinyanga, Raymond Kilindo, kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa manispaa hiyo, wakati akiwasilisha taarifa ya maandalizi ya miradi mitatu ambayo itafadhiliwa na benki hiyo.

Alisema WB inatarajia kutoa fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambayo ni ujenzi wa soko kuu la kisasa utakaogharimu Sh. bilioni 3.3, stendi ya mabasi (Sh. bilioni 4.5) na barabara za lami kilomita 18 (Sh. bilioni 27.7).

"Miradi hii yote mitatu inatarajiwa kuanza kutekelezwa kwenye mwaka wa fedha wa 2020/21) na itatoa ajira, kuboresha usafi wa mji, kukuza maendeleo, uchumi wa mji, miundombinu kwa wafanyabiashara kuwa rafiki na pamoja halmashauri kuongeza mapato," alisema Kilindo.

Naye Naibu Meya wa Manispaa, John Kisandu, alisema miradi hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya Shinyanga na kuwataka madiwani watoe ushirikiano wa kutosha ili ifanikiwe kuupanua mji na kukua kimaendeleo pamoja na kukuza uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

HUDUMA ZA TRA KWA NJIA YA MTANDAO

Ndugu mlipakodi TRA inakukumbusha kuwa, huduma zifuatazo zinapatikana kwa njia ya mtandao bila kulazimika kufika ofisini;-

1. Usajili wa TIN unaotumia namba ya kitambulisho cha taifa,
2. Makadirio na malipo ya kodi ya majengo,
3. Kujisajili kwa ajili ya kufanya malipo ya kodi moja kwa moja kupitia mfumo wa Revenue Gateway System na GePG,
4. Kuwasilisha kadhia za forodha kupitia mfumo wa TANCIS,
5. Kikokotoo cha magari yaliyotumika na kununuliwa kutoka nje ya nchi,
6. Kikokotoo cha kodi za ajira,
7. Minada kwa njia ya mtandao,
8. Maulizo na uwasilishaji malalamiko katika kituo cha huduma,
9. Kuchapisha cheti cha kodi ya zuio,
10. Uwasilishaji wa ritani za kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Kumbuka kuwa, unaweza kupata fomu mbalimbali kwa kutembelea tovuti yetu ya www.tra.go.tz

Kwa mawasiliano zaidi tufikie kwa kutumia mawasiliano yafuatayo;-

Simu za bure: 0800-750075 au 0800-780078

WhatsApp: 0744-233 333

Barua pepe: huduma@tra.go.tz

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

156808

# Eneo la kanisa ladaiwa kukwepa kodi ya ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

ENEO la Kanisa la Anglikana Mtaa wa Mtoni-Buza katika Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam, linedaiwa kutumika kukwepa kodi ya pango la ardhi kwa kuendesha biashara vikiwamo viwanda vinavyomilikiwa na raia kutoka China na maduka makubwa.

Hayo yalibainika jana baada ya Mkuu wa Kitengo cha Kodi kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masami, kutembelea eneo hilo lenye jumla ya ekari 410 ambalo limemilikishwa kwa matumizi ya makazi na si biashara.

Masami alifika katika eneo la taasisi hiyo baada ya kukaidi kulipa kodi ya pango la ardhi tangu mwaka 2005 na maofisa ardhi kutoka Manispaa ya Temeke wamekuwa wakipeleka hati za madai mara kwa mara bila kupewa ushirikiano wowote.

Kwa mujibu wa mkuu huyo, taasisi hiyo imebadili matumizi ya uendelezaji katika eneo hilo na kuweka wapangaji wanaofanya biashara mbalimbali.

Alisema katika baadhi ya maeneo, wameweka wapangaji kikiwamo kituo cha mafuta, zaidi ya maduka 200 ambayo yote yanafanya biashara, gereji, na viwanda vinavyozalisha bidhaa mbalimbali.

Kutokana na shughuli zote za kibiashara zinazofanywa katika eneo hilo la kanisa, alisema ni wajibu wao kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kuwa linatumika kibiashara tofauti na taratibu za umilikishaji ambazo zilihusu ibada.

Januari 29, mwaka jana, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alifuta kodi ya pango la ardhi kwa taasisi za dini na taasisi zingine zinazotoa huduma.

# Wafanyabiashara waonja machungu ya corona Dar

**Na Elizabeth Zaya**

UONGOZI wa soko la Mwananyamala umesema umeanza kuona athari za corona kwenye biashara zao kutokana na kupungua kwa wateja.

Akizungumza katika kipindi cha kumekucha kinachorushwa na kituo cha Televisheni cha ITV, Mwenyekiti wa Soko hilo, Mbaraka Saidi, alisema kwa sasa idadi ya wateja katika soko hilo imepungua kwa kiasi kikubwa tofauti na kabla ya kutangazwa kwa ugonjwa huo.

"Katika soko letu tumechukua tahadhari kulingana na tunavyoelekezwa na wataalamu wetu. Tumeweka kila mahali sehemu za kunawa wateja wetu wanapoingia kupata huduma," alisema Saidi.

"Lakini pamoja na kuchukua tahadhari hizo, tangu kutangazwa kwa ugonjwa huu wa corona, hali ya biashara siyo nzuri, wateja wanafika mmoja mmoja tena kwa tahadhari kubwa. Biashara za watu zimeharibika, hali ni mbaya," aliongeza.

Pia alisema hata baadhi ya wafanyabiashara sokoni hapo hawafungui kila siku biashara zao kutokana na uhaba wa wateja tofauti na ilivyokuwa awali hasa kabla ya kuripotiwa kwa ugonjwa huo nchini.

"Kutokana na kukosa wateja sokoni, baadhi ya wafanyabiashara wanakuja mara moja moja kwa ajili ya kufungua biashara zao, lakini mwingine anakuja leo lakini kuna wengine hawajafungua wiki nzima. Hali ni ngumu," alisema.

"Tangu umetokea huu mlipuko, kila mtu amekuwa na tahadhari ambayo hata wateja kuwa wengi imepungua, msongamano tuliokuwa tukiuona haupo tena, watu wanakuja kwa hofu wakiamini kwamba hili jambo ni la hatari."

Saidi alisema hali ya uchumi kwa wafanyabiashara katika soko hilo imeshuka na hivyo kuhatarisha mwenendo wa ulipaji wa ushuru.

"Mimi pia ni mfanyabiashara ndani ya soko la Mwananyamala huu mtikisiko ni mkubwa. Ndani ya soko hali ya uchumi imeshuka... kuna vitu ambavyo unaweza kufanya siri, lakini vingine vinaonekana wazi, hili ni janga na inavyotokea tatizo kama hili ni lazima mlibebe, kunapotokea mtikisiko huwezi kulazimisha mtu alipe ushuru hata kama hana cha kulipa," alisema Saidi.

Alisema wafanyabiashara wengi wanachukua bidhaa zao kwa gharama kubwa, lakini hawapati faida badala yake wanapata hasara.

"Mfanyabiashara kwa sasa anahangaika na yeye apate riziki, lakini biashara nazo zimeshakuwa ngumu, biashara nyingine ni za kuharibika, kwa mfano kwa sasa ananunua nyanya tenga Sh.40,000 anauza kwa Sh.10,000 utamdai nini tena katika hali hiyo, haya ni matokeo ambayo lazima tuyapokee kwa wakati huu."


Land Form No. 54 A

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE LAND ACT, 1999
(No. 4 of 1999)
DEFAULT NOTICE
(Under Section 127)

Title No 78945,
Plot No 95,
Block D,
Shariff Shamba Area,
Ilala Municipal,
Dar Es Salaam.

To: FRANK MICHAEL MREMA,
P O BOX 70036,
Dar Es Salaam.
(The Mortgagor)

That be notified of the default to honor your obligations, covenanted under the mortgage with Maendeleo Bank PLC, whereby you have guaranteed **NEW PAN GENERAL TRADING CO** who have failed to repay the loan facilities on due dates to the extent that, as of **March 19th, 2020 the outstanding balance is Tzs 107,540,281.44**

You are hereby required to pay the said Tzs 107,540,281.44 so as to rectify the said default. Please be informed that penalties and interest accrues daily

Be further notified that in the event you do not rectify the default stated above within Sixty (60) days from receipt of this notice, we may exercise our right to sell the mortgaged property/land cited above, or appoint a receiver, or lease the property, or enter possession or sue you in court.

Dated at Dar Es Salaam this 19th day of March 2020.

**FOR MAENDELEO BANK PLC**
**(THE MORTGAGEE)**
Served upon me at Dar es Salaam this……day of……………………2020
……………………………………
**Signature of borrower/Spouse/local authority/Guarantor**

MAENDELEO BANK PLC. P. O. Box 216, DAR ES SALAAM 19 MAR 2020 BRANCH MANAGER LUTHER BRANCH

**CC;** LILIAN LAWRENCE SHAYO T/A NEW PAN GENERAL TRADING CO.

215682902



MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA UMMA**

25 Machi, 2020

**UTARATIBU WA KUSAJILI VIPUKUSI CHINI YA MPANGO WA DHARURA WA KUPAMBANA NA UGONJWA WA HOMA KALI YA MAFUA UJULIKANAO KWA JINA LA COVID-19**

1. Kutokana na mlipuko wa homa ya Corona 2019 (COVID -19) ulioikumba dunia, ikiwemo Tanzania, matumizi ya vipukusi (antiseptics) hususan vitakasa mikono (hand sanitizers) yameongezeka. Hii ni kutokana na vipukusi hivyo kushauriwa kutumika kama njia mojawapo ya kuzuia kusambaa kwa virusi vinavyosababisha homa ya Corona. Aidha vipukusi vinavyotumika ni pamoja na vitakasa mikono vilivyotengenezwa kwa mchanganyiko wa "alcohol" (alcohol-based sanitizers), Chloroxylenol solution na Cetrimide + Chlorhexidine gluconate.

2. Kwa kuzingatia ongezeko la mahitaji ya vipukusi hivyo, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inapenda kuwafahamisha wale wote wanaojihusisha na utengenezji wa vipukusi kufuata utaratibu ufuatao:

2.1 Watengenezaji wa vipukusi wanaombwa kuwasilisha maombi ya usajili kwa mujibu wa taratibu za usajili wa vipukusi kama ambavyo zimeainishwa kwenye mwongozo wa usajili wa bidhaa hizo ujulikanao kama "Guidelines for Submission of Documentation for Marketing Authorization of Biocidals (Antiseptics and Disinfectants) Products, First Edition, February 2015" ambao unapatikana katika tovuti ya TMDA kupitia anuani ifuatayo (https://www.tmda.go.tz/publications/42.)

2.2 Maombi ya usajili yaambatane na nyaraka zote kama zilivyoainishwa katika mwongozo huo. Hata hivyo, iwapo baadhi ya nyaraka hazijaandaliwa au kukamilika wakati wa uwasilishwaji wa maombi hayo, waombaji wawasilishe taarifa chache zifuatazo:-
a) Fomu ya maombi (Application form)
b) Kanuni ya mchanganyiko wa kitakasa (Composition formula)
c) Hati ya uchunguzi (Certificate of analysis) endapo ipo
d) Lebo ya bidhaa (Labelling information)

Pamoja na nyaraka tajwa hapo juu, mwombaji atapaswa kuwasilisha barua ya ahadi yenye sahihi na tarehe kuthibitisha kwamba taarifa zilizosalia zitawasilishwa hapo baadaye.

2.3 Kuhusu utengenezaji wa vitakasa mikono (hand sanitizers), wazalishaji ambao wamesajiliwa pamoja na mahospitali na famasi wafuate mwongozo wa utengenezaji wa vitakasa mikono uliondaliwa na ujulikanao kama "Guidance for Production of Alcohol – Based Hand Sanitizers under Public Health Emergency Preparedness" unaopatikana kwenye tovuti ya TMDA **(www.tmda.go.tz).**

2.4 Maombi ya usajili yawasilishwe katika ofisi ndogo za makao makuu ya TMDA zilizoko barabara ya Mandela eneo la Mabibo External, Ubungo, Dar es Salaam au kwenye ofisi za Kanda.

3. Baada ya kupokea maombi ya usajili, TMDA itafanya tathmini ya haraka ya maombi hayo na kutoa majibu ya tathmini hiyo ndani ya siku tatu (3) za kazi tangu kuwasilishwa kwa nyaraka za maombi.

4. Kwa pamoja tushirikiane kupamba na ugonjwa huu hatari.

**Imetolewa na:**
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba,**
**S.L.P 1253, Dodoma Au**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam**

**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751**
**Barua Pepe: info@tmda.go.tz**
**Simu bila malipo: 0800110084**

215681902

HABARI KITAIFA

# Waomba mfumo uuzaji korosho ghafi uangaliwe

Na Mwandishi Wetu, MTWARA

UONGOZI wa kiwanda cha kubangua na kuchakata korosho cha Yalin Cashewnut Company Limited kilichoko mkoani Mtwara, umeiomba serikali kuweka utaratibu mwingine wa uuzaji wa korosho ghafi, ili kuwawezesha wenye viwanda vya kuchakata korosho nchini kupata mali ghafi hiyo kirahisi na kwa bei nafuu.

Hatua hiyo inatokana na malalamiko yaliyotolewa juzi na Meneja Mkuu wa Kiwanda hicho, Sulaiman Millanzi, aliyesema utaratibu uliopo kwa sasa, unawataka wenye viwanda kununua mali ghafi hiyo kupitia minada ambayo wanakumbana na ushindani mkubwa wa bei kutoka kwa wanunuzi ambao wanasafirisha korosho ghafi kwenda nje ya nchi.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, imeweka utaratibu mpya wa uuzaji na ununuzi wa mazao ya biashara hususani korosho, ikiwataka wanunuzi wote wa mazao hayo kununua kupitia minada inayofanyika kwenye vyama vya ushirika nchini, lengo likiwa ni kuhakikisha wakulima wananufaika na bei ya mazao yao.

Mwaka wa fedha 2018/19, serikali ilipanga bei elekezi ya Sh. 3,300 kwa kilo ya korosho na kuwataka wanunuzi wote kununua korosho za daraja la kwanza kwa bei hiyo, uamuzi ambao ulisababisha wanunuzi wengi kugomea kununua zao hilo kwa kisingizio kwamba bei elekezi ilikuwa kubwa na wasingeweza kupata faida wakati wa kuuza.

Baada ya mgomo huo, serikali kupitia Jeshi la Wananchi, chini ya maagizo ya Rais John Magufuli, ilinunua korosho zote zaidi za tani 200,000 kutoka kwa wakulima.

"Kwa sasa, tunanunua korosho ghafi kupitia mfumo wa Bodi ya Korosho unaotambulika na serikali, korosho zinauzwa minadani, hivyo, sisi wenye viwanda tunakwenda kwenye minada kushindana na wanunuzi wanaonunua na kusafirisha nje ya nchi.

"Kwetu sisi kama wachakata korosho ambao tunatoa ajira kwa Watanzania na kulipa kodi kwa serikali, hili ni kikwazo, kwani inapotokea wanunuzi wote wa ndani na wa nje tunanunua korosho kwa bei sawa, mfano Sh. 3,000 au Sh. 4,000, kwetu sisi inatugharimu na inaweza kuua biashara zetu," alilalamika.

Milanzi alitoa malalamiko hayo mbele ya maofisa wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) ambao juzi walikitembelea kiwanda hicho wakati wa ziara yao ya kikazi mkoani Mtwara.

Vilevile, alisema kiwanda hicho kilichojengwa eneo la Viwanda la Msijute, takribani kilometa 10 kutoka mjini Mtwara, kina uwezo wa kuchakata tani 6,000 kwa mwaka na kimeajiri Watanzania 600, wengi wao ni wanawake.

"Tunatarajia kuongeza uzalishaji kufikia tani 10,000 hivi karibuni baada ya kufunga mashine zingine. Wafanyakazi wetu wengi ni wanawake kwani ndiYo waaminifu na wanafanya kazi kwa kujituma zaidi kulinganisha na wanaume ambao hawazidi asilimia 15 ya wafanyakazi wote hapa kiwandani.

"Wafanyakazi wanaume kazi zao zinahusisha hasa kubeba vitu vizito na kazi zingine za kutumia nguvu," alibainisha.

Kwa upande wa masoko, Millanzi alisema kiwanda hicho kinauza korosho iliyochakatwa na kuhifadhiwa kwenye vifungashio vya kilo 22 na kuuzwa China.

"Korosho zetu tunaziuza China ambako ndiyo kuna soko kubwa. Tayari tushapokea oda kutoka kwa wanunuzi wetu China. Kusema ukweli, soko ni kubwa sana China, hatujawahi kukosa soko," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kushoto), akizungumza na mmoja wa wauzaji wa maji kwa wananchi kwenye vituo ambavyo vimetengwa katika Kijiji cha Lyabusalu, katika Halmashauri ya Wilaya hiyo, akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maji juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wawakilishi wataka watumishi kutimiza wajibu

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

KAMATI ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi imeeleza kuridhishwa na utendaji kazi wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kisiwani Pemba, na kuishauri kusimamia utendaji wa watumishi.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othman Said, wakati wa majumuisho ya Kamati hiyo baada ya kutembelea taasisi mbalimbali zilizoko chini ya wizara hiyo.

Alisema kuwa kamati imeridhishwa na utendaji mzuri wa wizara hiyo na kueleza kuwa ofisi hiyo ina wajibu wa kuhakikisha kuna usawa na haki kwa watumishi wa serikali.

"Tumeona jitihada kubwa zilizochukuliwa na Rais wetu kwa kuimarisha maslahi bora kwa watumishi wote wa umma... hivyo basi wizara hii inatakiwa isimamie kwa karibu ili mtumishi aweze kupata haki yake kwa mujibu wa sheria na taratibu," akisema na kuongeza: "Na aweze kufanya kazi katika mazingira mazuri ili na yeye afanye kazi kwa uadilifu na kwa weledi mkubwa."

Hata hivyo, Machano aliitaka wizara hiyo kuendelea na ukaguzi kwa watumishi pamoja na uhakiki ili kutambua wanaopashwa kuwapo pamoja na kuangalia maslahi yao kwani hilo ni jambo muhimu na ni la lazima katika taasisi zote za serikali.

"Wito wetu ni kwamba zoezi hili la uhakiki kwa watumishi wa taasisi zote za serikali liendelee na mzidishe kasi ili muweze kutambua waajiriwa waliomo katika taasisi zetu," alieleza mwenyekiti huyo.

Kadhalika, Machano alielezea wajibu wa watumishi ni kufanya kazi wanazopangiwa badala ya kutegemea tu kupata mshahara, hivyo aliiomba wizara hiyo kusimamia na kuhakikisha watumishi wanatimiza wajibu.

Nao wajumbe wa kamati hiyo waliipongeza wizara hiyo kutokana na kazi kubwa wanayoifanya na kuwataka kuendelea kushirikiana katika majukumu yao.

# Wanafunzi wapata ukombozi wa maji

Na Julieth Mkireri, BAGAMOYO

WANAFUNZI 320 wa Shule ya Sekondari ya Mapinga, wilayani Bagamoyo Mkoa wa Pwani, wameondokana na kero ya maji baada ya taasisi moja kwa kushirikiana na shule za Feza, kutekeleza mradi wa uchimbaji kisima katika shule hiyo.

Taasisi hiyo ni It's Time to Help Foundation Tanzania, ambapo hafla ya makabidhiano ya mradi huo ilifanyika shuleni hapo juzi, baada ya mradi huo uliogharimu Sh. milioni 12, kukamilika na kukabidhiwa kwa uongozi wa shule hiyo.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Ofisa Uhusiano wa Taasisi hiyo, Mbwana Kitendo, alisema taasisi hiyo ina utaratibu wa kutoa misaada kwa jamii katika sekta za afya, elimu na sekta ya ustawi wa jamii na vituo vinavyohudumia watoto.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Julius Mwanganda, alishukuru taasisi hiyo kwa kuona uhitaji uliokuwapo shuleni hapo na kuwa tayari kutoa msaada huo kwa shule hiyo ambayo ilikuwa na changamoto ya ukosefu wa maji.

Alisema, ukosefu wa maji katika shule hiyo ulikuwa ukisababisha usumbufu kwa walimu na wanafunzi.

Mkuu wa shule hiyo, Agnes Mmbaga, alisema, awali walikuwa wakitumia maji kutoka katika kisima cha kuchimba kwa mkono kilichochimbwa na walimu pembezoni mwa shule hiyo, ambacho hakikuwa na maji ya uhakika na hayakuwa salama kiafya.

"Kukosekana maji katika shule yetu kulisababisha kupoteza muda mwingi kutafuta maji, badala ya kutumia muda huo kwenye masomo, mradi huu ni ukombozi kwa wanafunzi na walimu wa shule yetu, tunaahidi kuutunza," alisema Mmbaga.

Mmbaga, alisema kwa sasa wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa, uzio, umeme, maabara, maktaba, matundu ya vyoo na ofisi ya walimu, huku akiwaomba wadau wa elimu kusaidia kutatua kero hizo.



Mafundi wakifyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Mkapa, iliyopo katika kijiji cha Kastam, Kata ya Bukima Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ambayo kwa sasa ina madarasa 10 na yanahitajika mengine 14. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# TIC kumpa mwekezaji eneo mbadala kiwanda cha sukari

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kushirikiana na serikali mkoani Mtwara, wameahidi kumtafutia eneo mbadala mwekezaji wa kilimo cha miwa ili aweze kujenga kiwanda cha sukari.

Uamuzi huo unatokana na kujaa maji na kuharibu miundombinu eneo lote alilopewa awali.

Mwekezaji huyo wa Kampuni ya SJ Sugar Distillery & Power Private amehakikishiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe, aliyefanya ziara ya ghafla kwenda kujionea uharibifu mkubwa wa miundombinu ya eneo hilo kufuatia mvua kubwa zinazoendelea nchini.

Akizungumza na waandishi baada ya kutembelea eneo hilo mla mwekezaji lililopo Kilambo, Mwambe alisema athari za mvua katika eneo la uwekezaji ni kubwa kutokana na zaidi ya miche 300,000 ya miwa kuharibika kwa sababu ya mafuriko katika eneo hilo.

"Wawekezaji hawa walishaanza kazi kwa kupanda miche kwenye eneo la hekari 500 kati ya hekta 3,000 walizopewa kufanya uwekezaji, lakini eneo lote limeharibiwa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha," alisema Mwambe.

Alieleza kuwa TIC imefanya jukumu la kuwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara kwa lengo la kumpatia eneo jingine mwekezaji ili aendeleze mradi wake ambao utakuwa na faida katika mikoa ya kusini na taifa kwa ujumla.

"Tumeambiwa kiwanda kitakapo kamilika kitaweza kuzalisha sukari tani 10,000 jambo ambalo litasaidia kupunguza uagizaji wa bidhaa hiyo nje ya nchi," alisema Mwambe na kuongezea kuwa TIC itawajibika kuhakikisha mwekezaji anapata eneo lingine la kuwekeza mradi wake mapema iwezekanavyo.

Mwambe alisisitiza kuwa azma ni kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025, hivyo TIC inawajibu wa kufanikisha azma hivyo inatimia pamoja na kumwezesha mwekezaji wa kiwanda cha sukari kunapatiwa eneo lingine la kuwekeza.

"Ipo haja kwa mwekezaji huyu kutafutiwa eneo mbadala la kufanyia uzalishaji kutokana na eneo la sasa kukumbwa na mafuriko, hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji," alisema Mwambe.

Alisema kiwanda hicho kitakuwa cha kwanza kwa kanda ya kusini na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha ajira nyingi na hasa kwa vijana na pia kupunguza kiwango cha uagizaji wa sukari nje ya nchi, jambo ambalo litasaidia kukuza pato la nchi. Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evod Mmanda, alisema atashirikiana na watendaji wake kuwa eneo mbadala watakalopewa wawekezaji hao linafanyiwa tathmini zote kabla ya kuwakabidhi.

Naye Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Kamel Abdullah Saleem, alipongeza hatua za haraka zilizochukuliwa na TIC pamoja na Serikali ya Mkoa kwa kuwatembelea na kuahidi kuwapatia eneo lingine kwa ajili ya kuendelea uwekezaji wao.

# Kesi ya mfanyabiashara, askari leo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MFANYABIASHARA maarufu jijini Arusha, Shabiby Virjee (34), na wenzake wawili, akiwamo askari polisi wanaokabiliwa na kesi ya kuomba rushwa ya Sh. milioni 10, inatarajiwa kuanza kusikilizwa leo katika Mahakama ya Wilaya ya Arusha.

Kesi hiyo awali ilipangwa kusikilizwa Februari 8, mwaka huu, kwa watuhumiwa kusomewa maelezo ya awali, lakini ilishindikana kusikilizwa baada ya wakili wa mshtakiwa wa kwanza, Gwakisa Sambo, kushindwa kufika mahakamani hapo, na kuomba kuahirishwa hadi leo.

Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Nestory Baro, alisema watuhumiwa wataanza kusomewa maelezo ya awali.

Waendesha mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Arusha wamekamilisha upelelezi wa kesi hiyo, na wapo tayari kuanza kusikilizwa kwa kesi hiyo.

Mbali ya Virjee, wengine walioshtakiwa katika kesi hiyo ni pamoja na aliyekuwa askari polisi Kituo Kikuu cha Polisi Arusha, Paulo Erasmo (37) na mfanyakazi wa kampuni ya mafuta ya Oryx, Nkenzi Pazi (38).

Mfanyabiashara huyo na wenzake wanaotetewa na wakili Godluck Maico na Sambo Gwakisa, wanakabiliwa na shtaka moja la kutoa rushwa ya Sh. milioni 10, ili kumpatia askari polisi Meshack Laizer, aliyekuwa amewakamata wafanyakazi wawili wa kampuni ya mafuta ya Oryx wakidaiwa kuuza mafuta uchochoroni kinyume cha sheria.

## Serikali yajipanga kuibua wabunifu

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema inatafuta namna bora ya kuweka mikakati ya kuwaibua wabunifu na kuwasaidia kuendeleza bunifu zao.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu, alisema lengo ni kuhakikisha wanaingia sokoni badala ya kazi hizo kubaki kuwa za maonyesho pekee.

"Tunahitaji kubadili mawazo yetu ili kufikia malengo, ubunifu unatakiwa kuleta mabadiliko katika jamii yetu, tunahitaji kubuni kwa manufaa na ndiyo maana tunatakiwa kutengeneza mikakati maalum ya kuwaibua wabunifu," alisema Dk. Nungu. "Tunatakiwa kuisaidia Tanzania hususani katika kipindi hiki inapojenga na kuimarisha uchumi wa viwanda, tutumie vijana wetu ambao kwa sasa wameikubali sekta hii ya ubunifu kuleta mapinduzi ya teknolojia na nimefurahi sana kuona wameingia kwa wingi."

Alisema mwaka huu kiwango cha kazi za kibunifu kimeongezeka tofauti na ilivyokuwa mwaka jana na kwamba lengo ni kuhakikisha ubora huo unaongezeka zaidi.

Kwa mujibu wa Dk. Nungu, kila mwaka wanapokutanisha wadau wa sayansi ya ubunifu wamekuwa wakijifunza mambo mapya na namna ya bora ya kuboresha.

"Mwaka huu pia tumeona kuna mabadiliko makubwa katika sekta hii ya sayansi ya ubunifu, tutaendelea kujifunza na kuboresha na tunaamini kwamba huko mbele tuendako mambo yatakuwa mazuri zaidi, lengo kubwa tunataka sekta hii ilete impact," alisema Dk. Nungu.

"Miaka ya nyuma tulikuwa tunaona wanaoingia katika sekta ya ubunifu ni wanaume tu, lakini miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia hata vijana wa kike nao wameamua kushindana na wenzao wa kiume, ni jambo la kujipongeza na lazima tuhakikishe kwamba tunawashika mkono."

# Tughe yaifagilia serikali hatua corona

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (Tughe) mkoani Manyara, kimeipongeza serikali kwa jitihada inazozichukua katika kupambana na ugonjwa wa corona ambao umekuwa janga la dunia. Pongezi hizo zilitolewa jana mjini hapa na Mwenyekiti wa Tughe mkoani Manyara, Honest Temba, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu namna serikali inavyochukua hatua katika kuhakikisha ugonjwa huu unadhibitiwa.

Alisema chama hicho kinatambua juhudi kubwa inayofanywa na serikali ya kuwaelimisha wananchi na wafanyakazi njia sahihi za kuepukana na ugonjwa huo.

"Kwa mkoa wetu ofisi nyingi zimechukua tahadhali ikiwa ni pamoja na kuweka ndoo zenye majisafi ya kunawia mikono, lakini vitakasa mikono (sanitizer) kimsingi juhudi za serikali zinaonekana," alisema Temba.

Aidha, alisema pongezi ziende kwa viongozi ngazi za juu yaani Rais John Magufuli, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Waziri wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kwa kuongoza jitihada za kutoa elimu kwa Taifa.

Naye Katibu wa Tughe mkoani humo, Saburi Katamulo, alisisitiza wanachama wao na watumishi kwa ujumla kuzingatia maelekezo kutoka Wizara ya Afya, ikiwamo kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kushikiana.

Aliwataka wauguzi na madaktari, ikitokea wakampokea mgonjwa ambaye anadhaniwa kuwa na ugonjwa huo, wamhudumie kadri taaluma yao inavyowataka bila kumnyanyapaa.

Alisema wanawasisitiza wanachama wao katika matawi yao, kununua vitakasa mikono, lakini kujikita katika kutoa elimu dhidi ya mapambano ya ugonjwa huo.

Katibu wa Kamati za Wanawake wa Tughe mkoani hapo, Veronica Paulo, aliwataka wanawake kuwa makini katika jambo hilo na kuchukua tahadhali kubwa kwao na kwa watoto.

Alisema hatafurahi kusikia kuna mwanamke wa Tughe amepatwa na ugonjwa huo, kwa kuwa wanawake wanategemewa na familia katika masuala ya maendeleo na Taifa kwa ujumla hivyo ni vizuri wachukue tahadhari.



Wajasiriamali Anusiathа Raphael (kushoto) na Tea Vitalia, wakionyesha baadhi ya vyakula vinavyopikwa na kikundi chao cha Themi Living Garden, kilichopo katika eneo lenye mandhari nzuri yenye kuvutia watalii katikati ya msitu wa Themi, jijini Arusha juzi. Walisema kuwa tangu waanzishe kikundi hicho, kimekuwa msaada mkubwa kwao kwani sasa wanaweza kutunza familia zao kutokana na kipato cha biashara hiyo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Kesi ya kigogo OBC yapigwa kalenda

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, juzi ilishindwa kuendelea na kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Otterlo Business Limited (OBC), Isaya Mollel.

Kampuni hiyo inamilikiwa na mwanamfalme wa Falme za Kiarabu, kutokana na upelelezi wa kesi hiyo kutokamilika.

Akiomba kuahirishwa kwa kesi hiyo, Wakili wa Serikali, Ahmed Khatibu, mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Martha Mahumbuga, alidai kuwa, upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

"Mheshimiwa Hakimu, tunaiomba mahakama hii tukufu iahirishe kesi hii na kupanga tarehe nyingine kwa sababu upelelezi wake haujakamilika," alisema. Baada ya Wakili Khatibu kuwasilisha ombi hilo, Hakimu Martha alilikubali ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Aprili 4, mwaka huu itakapotajwa tena na kuamuru mtuhumiwa kurudishwa mahabusu katika Gereza Kuu la Kisongo jijini Arusha.

Mollel anakabiliwa na makosa 10, likiwamo la ukwepaji kodi na utakatishaji fedha haramu na kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 12.4.

Mollel ni miongoni mwa watuhumiwa walioandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kuomba kukiri mashtaka yanayomkabili.

Mollel alikamatwa Februari 21, mwaka juzi na tangu akamatwe hajawahi kupata dhamana, kutokana na kesi hiyo kutokuwa na dhamana.

# Wadau wasaidia vita dhidi corona

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WADAU wa maendeleo mkoani Arusha, wametoa misaada ya vitakasa mikono vyenye thamani ya Sh. milioni 3.9 kwa ajili ya kusaidia kukabiliana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Akikabidhi msaada huo jana kwa uongozi wa mkoa wa Arusha, Meneja wa Kampuni ya Planet Phamasetcal Limited, Joseph Lekumok, alisema msaada huo ni sehemu ya mchango wa kusaidia kukabiliana na ugonjwa huo ambao ni janga la ulimwengu.

Alisema wameona wao kama wadau kuna kila sababu ya kusaidia serikali kupambana na ugonjwa huo kwa kutoa msaada.

Akipokea msaada huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema mkoa bado unahitaji misaada mbalimbali ikiwamo vitakasa mikono, kwa ajili ya kujikinga wananchi dhidi ya maambukizi ugonjwa wa corona.

Aliwapongeza baadhi ya wadau ikiwamo Benki ya CRDB na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kwa misaada yao katika kukabiliana na ugonjwa wa corona, na kuwaomba wadau wengine kutoa misaada yao.

Kuhusu mkoa kutekeleza maelekezo ya kutenga maeneo maalumu ya wagonjwa wa corona kutoka kwenye nchi zenye ugonjwa huo, alisema mkoa umeshatenga maeneo ya kutosha kwa ajili ya wote watakaogundulika kuwa na maambukizi ya corona.

Alisema wote watakaokutwa na maambukizi watawekwa kwenye maeneo hayo yaliyotengwa ambayo watakaa humo kwa siku 14 kwa gharama zao wakati wakipata matibabu mpaka wataalamu wa afya watakapoona afya zao zimetengemaa, lengo ni kuzuia maambukizi kwa wengine.

Kwitega alisema hadi kufikia Machi 24 mkoa ulikuwa haujapokea mgonjwa wa corona na serikali inaendelea kufuatilia taarifa kwenye maeneo yote ya mipakani na iwanja vya ndege, ili kuwatambua na kuwadhibiti wote wanaoingia nchini kama wana maambukizi ya corona.





# Amcos walia na mwekezaji

**Na Mary Mosha,** HAI

WANACHAMA wa Chama cha Msingi cha Ushirika wa Mazao cha Nkuu (Nkuu Amcos), wameiomba serikali kuingilia kati juu ya mwekezaji aliyejimilikisha shamba lao lenye ukubwa wa ekari 300 bila kufuata utaratibu hali inayotishia hali ya chakula kwa wanachama hao.

Wakizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika chama kikuu cha Nkuu na kuhudhuriwa na wanachama wapatao 1,400 walisema kuwa shamba lao la Mkufi lina ukubwa wa zaidi ya ekari 700 na kuwa ekari 400 zimekodishwa kwa wawekezaji.

Askofu mstaafu John Elichilia, mwanachama alisema walishangaa mwekezaji huyo kuchukua ardhi hiyo bila kufuata utaratibu kama walivyofanya wawekezaji wengine na kuwa ardhi hiyo ilibakizwa kwa ajili ya kilimo kwa wananchi.

Alisema kumetumika njia zisizoeleweka kwa mwekezaji huyo kujimilikisha ardhi hiyo, huku wanavijiji wa vijiji viwili vya Nkuu Sinde na Nkuu Ndoo wakikosa ardhi kwa ajili ya kuendeshea kilimo cha kujikimu kama ambavyo wakifanya kipindi cha nyuma.

''Mwekezaji kaja hapa kwa njia ambazo hatujashirikishwa sisi wanachama hatujui tutalima wapi na watoto wetu katika shule tatu zinazotuzunguka hapa watakula nini tunaomba serikali hii sikivu itusaidie,'' alisema.

Fadhila Mushi miongoni mwa wanachama alisema kipindi cha nyuma wakati wawekezaji wanakuja walikubaliana wabakize ardhi ambayo itawasaidia wanavijiji hao na hilo lilifanikiwa kabla ya kuja kuvamiwa na mwekezaji huyo.

Alisema mwekezaji huyo ambaye alifahamika kwa jina moja tu la James ni kama kapora ardhi hiyo kwa kuwa hata viongozi wa bodi ya vyama vya msingi hawaoneshi kuchukua hatua yoyote katika kumwondoa katika shamba hilo.

Rajab Nkya, alisema kuwa kuna kila haja ya serikali sikivu ya awamu ya tano kuingilia kati tofauti na hapo ni kuwanyima wanachama mali yao walioimiliki kwa kipindi kirefu na hatimaye kuporwa na watu wachache.

Alisema kilichoonekana ni kama jitihada za kikundi cha watu wachache wenye tamaa ya mali kughushi nyaraka ili kuonekana mwekezaji ni mmiliki halali na alifuata sheria jambo ambalo halina ukweli wowote.

Mwenyekiti wa bodi ya chama hicho, Isai Shoo, alipoulizwa juu ya tuhuma hizo za ukodishwaji wa shamba bila kufuata utaratibu alisema kuwa hawezi kuongea kwa kuwa kuna kazi inaendelea.

"Kwa sasa ni jioni sana muda wa kazi umeisha na sitaweza kuzungumza na waandishi wa habari, lakini hata hivyo kuna kazi ambayo inaendelea kuhusu hilo suala," alisema.

# Kampuni za Kenya kusaidia wakulima

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMPUNI mbili za kimataifa kutoka nchi jirani ya Kenya, zitaanza kuwafuta machozi wakulima wa mazao ya mboga na nafaka wa vijiji vya pembezoni kati ya Wilaya ya Moshi na Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa vikilalamikia kukosa soko la uhakika la mazao.

Jana, Meneja Miradi wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Rikolto inayowasaidia wakulima nchini kupata masoko ya uhakika, Kain Mvanda, alisema kampuni hazi zipo tayari kununua tani 180 kwa mwezi.

Mvanda alitangaza neema hiyo kwa wakulima hao, baada ya kukutana na kuafikiana na menejimenti za Kampuni ya Fresh Mart na Molly Flowers ya Kenya ambayo yananunua mazao ya mboga kwa wakulima.

"Baada ya kusikia kilio chenu ambacho mmesema ni cha muda mrefu, Rikolto tulichukua hatua katika kuwasaidia wakulima mnaovuja jasho kupata stahiki zenu kama kuongeza kipato kupitia kilimo hiki. Sasa, makampuni hayo yapo tayari kununua tani 180 kwa mwezi, sawa na kilogramu 180,000.

"Wametuhakikishia kwamba wako pia tayari kuendelea kuongeza kiwango cha tani cha ununuzi wa mazao yenu, lakini wakizingatia ubora wa mazao ya mboga mnayolima ama kustawisha."

Kwa mujibu wa Mvanda, hivi sasa kampuni hizo tayari zimeanza mchakato wa kuonana na wakulima na taasisi zinazowasaidia wakulima, na kuingia mikataba ya ununuzi wa mazao hayo.

Aidha, alisema wakulima wa Tanzania wamekuwa wakikabiliwa na tatizo kubwa la masoko ya mazao ya mboga wanayolima na hivyo kuwasababishia wengine kukata tamaa ya kuendelea na kilimo hicho.

Alisisitiza kuwa ujio wa kampuni hizo za kununua mazao ya wakulima, utasaidia kutatua kero ya muda mrefu ya mazao kukosa masoko.

Viongozi wa kampuni hizo zinazonunua mazao ya mboga na matunda kwa wakulima kutoka nchini Kenya, Gibson Ngondo ambaye ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Fresh Mart na Warmolt Tonckens ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Molly Flowers kwa nyakati tofauti, wameeleza kuwa wanao uwezo wwa kununua mazao hayo kwa wakulima.

"Tuko tayari kuingia mikataba, bila ya kujali bei inapopanda na kushuka, tutakuwa tunanunua mazao hayo kwa gharama ambazo tutakuwa tumekubaliana," alikiri Ngondo ambaye ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Fresh Mart.

Wiki iliyopita, wakulima wa vijiji vya Msitu wa Tembo na Londoto vilivyoko Wilaya ya Simanjiro, na Langasani, Mikocheni na Arusha Chini vilivyoko Wilaya ya Moshi, walinukuliwa na Nipashe wakidai kuwa kukosekana kwa soko hilo, kusababisha hasara kubwa kwa wazalishaji ambao hutumia gharama kubwa kuzalisha na kushindwa kuuza.



Mmoja ya wajasiriamali wadogo, Jonathan Mapunda kutoka Vivian Boutique akishona nguo za vitenge mjini Moshi jana, kwa ajili ya wateja wake ambao wengi ni watalii wanaokwenda kupanda Mlima Kilimanjaro. Mapunda alilalamikia kupungua kwa kiwango kikubwa cha watalii kutokana na tishio la ugonjwa wa corona. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mjane aiangukia serikali kuporwa ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MJANE Anna Sebastian (80), mkazi wa Kijiji cha Wiri katika Wilaya ya Siha, ameiomba serikali kuingilia kati mgogoro wa shamba unaofukuta kati ya
na Menejimenti ya Shamba la Molomo, baada ya watu kadhaa kudaiwa kuvamia ardhi yake na kufyeka mazao ikiwamo miti.

Akizungumza na Nipashe jana kijijini hapo, bibi huyo alidai kuwa watu hao walioagizwa na menejimenti ya shamba hilo, walivamia siku chache zilizopita shamba lake na kuharibu mazao yake, kwa madai kuwa eneo hilo ni miliki ya shamba hilo na anapaswa kuondoka.

Kutokana na mgogoro huo kufukuta, kikongwe huyo ameiomba serikali wilayani humo kuviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuwakamata kwanza walioharibu mazao yake na kutafuta ukweli juu ya umiliki wa ardhi hiyo.

Akiwa katika eneo hilo, bibi huyo ambaye ni mjane, alidai eneo la shamba lake lina ukubwa wa ekari tano na lililoharibiwa ni nusu ekari.

"Wajukuu zangu, hili shamba nilipewa enzi za ukoloni na mzungu aliyekuwa anaitwa 'Kajogoo' alikuwa anamiliki shamba la Molomo na mimi nilikuwa mfanyakazi wa shamba hilo.

"Hili eneo tulipewa na wakoloni mwaka 1969 kama zawadi, kwa kuwa tulikuwa wafanyakazi wa shamba hilo. Lilikuwa pori kubwa walituambia tufyeke tujenge, hatukuwa wenyewe, tulikuwa na wafanyakazi wengine."

Aliongeza: "Mwaka 1984, Chama Kikuu cha Ushirika wa Kahawa mkoani Kilimanjaro (KNCU), walitupa kielelezo cha kutambua kwamba eneo ni letu na tunaruhusiwa kufanya shughuli zote, lakini hawa watu wanatufuata wanatunyanyasa, tunaomba Rais John Magufuli na wasaidizi wake waingilie jambo hili, kwa kuwa serikali yake inajali wanyonge."

Alisema chokochoko zilianza mwaka jana, baada ya maofisa wa Shamba la Molomo Farm kufika kwenye eneo lake na kudai ni eneo lao, wakimtaka aondoke yeye na familia yake na waliwapeleka Kituo cha Polisi Sanya Juu.

Msaidizi wa Kisheria anayefanya kazi na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization (Kwieco) ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Wiri, Hamza Munisi akizungumzia sakata hilo alisema kitendo walichofanya watu hao sio cha kiungwana, hasa ukichukulia mjane huyo alipewa ardhi hiyo na wakoloni.

Kwa mujibu wa Hamza, mjane huyo ameishi katika ardhi hiyo kwa zaidi ya miaka 40 sasa bila bughudha yeyote.

Alipotafutwa Meneja wa Shamba hilo, Peter Ngatia, alikiri kuwa wao ndiyo waliohusika kufyeka mazao hayo, kwa kuwa kuna mtu amevamia eneo lao.



## Mradi nishati jua 'unaowatoa' wenye ulemavu shimoni, wakaibukia kwenye ujasiriamali

Ukurasa 14


# BUFE

Ijumaa Machi 27, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## Ijue programu inayowafanya vijana kujitambua kiuchumi

Ukurasa 20



# MWALONI:
# Soko la kimataifa ufukweni mwa Ziwa Victoria lililosheheni bidhaa sangara

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

BIASHARA

# Mradi nishati jua 'unaowatoa' wenye ulemavu shimoni, wakaibukia kwenye ujasiriamali

## • Orodha ya vijiji tabasamu, ila ombi...

**Na Beatrice Philemon**

KUNA namna mradi ambao ni maarufu kama 'Solar Mtaji Programme' au unavyotamkwa 'Sola Mtaji' ulivyobadilisha maisha ya wananchi, wakiwamo watu wenye ulemavu.

Unapozungumzia mradi huo kwa lugha ya kawaida, ni endelevu kibiashara unaogusa jamii moja kwa moja katika shughuli za kila siku, kuipa familia uhakika wa maisha.

Ni mradi uliozinduliwa rasmi mwaka jana, wa ajili ya kusaidia vikundi vya vijana, wanawake, wajane, walemavu na mtu mmoja mmoja katika maeneo wanakoishi, kwa kutumia umeme wa nishati ya jua.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Uhusiano wa kampuni ya Sepon, Frank Swai, anasema lengo ni kuhakikisha wanawatengenezea mazingira mazuri ya kujipatia kipato kwa uendeshaji wa biashara, hatua itakayowasaidia kupata mbinu mbadala za kukabiliana na ugumu wa maisha na kuepukana na utegemezi.

**MAFANIKIO YAKE**

Anasema Sola Mtaji inabeba maana: "Sisi hatukupi fedha, hatukopeshi fedha, ila tunakutengenezea mazingira yaliyo rafiki kwa kukupatia nyenzo ya kufanya biashara au nyenzo ya uendeshaji biashara itakayo kuongezea kipato cha ziada (mlo wa pili) ndani ya familia au jamii hali itakayosaidia kutokomeza manyanyaso ya kijinsia kwa wanawake."

Swai ana angalizo kuwa, itasaidia kutokomeza unyanyasaji wanawake kijinsia, kwa kutokuwa na uamuzi wa uzalilishaji, hata ikaibua migogoro ya ndoa za kila mara.

Anasema, mpaka sasa mradi umeshafikia wanachama 82 kutoka vikundi vitatu, kikiwemo cha walemavu kilichoko katika kijiji cha Lukooni, kata ya Chanika, wilayani Ilala, kinachojulikana kama 'Umoja wa Kusaidiana Walemavu-kata ya Chanika (Ukwacha),

Pia, anataja katika kijiji cha Kibindu, katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze na kikundi cha wanawake kilichopo Magomeni wilaya ya Kinondoni.

"Lengo letu ni kufikia vijana 1000 nchi nzima ifikapo mwaka 2021 kupitia mradi huu," anasema Swai, kampuni hiyo ikilenga kuwapa mafunzo ya bure wananchi na nyenzo za kufanyia kazi.

"Tuliamua kujikita katika mradi huu ili kujaribu kubadilisha mtazamo wa wananchi, badala ya wananchi kutumia umeme wa nishati ya jua kupata mwanga, kutizama TV, kusikiliza radio, sasa tunawatoa eneo hili na kuwaleta kwenye sekta ya ufanyaji biashara ambayo itamsaidia mwananchi kipato ndani ya familia," anasema

Anasema, kupitia mradi mwananchi anapata ada za wanafunzi, nauli za shule, chakula, maziwa ya mtoto , huduma za afya, kuanzisha miradi na huduma nyingine za kijamii.



Katibu wa kikundi cha Umoja wa Kusaidiana Walemavu Kata ya Chanika (Ukwacha), Amina Kisembe, akishona nguo kwa kutumia cherehani inayotumia umeme wa nishati jua, pembeni yake ni Fundi Zuhura Mkone, akimuelekeza.

Swai anasistiza nishati ya jua imesaidia vijiji mbalimbali kuanzisha miradi mbalimbali, kwa ajili ya kujiongezea kipato na kupambana na umasikini.

"Kwa mfano, kikundi cha Umoja wa Kusaidiana Walemavu-kata ya Chanika (Ukwacha) tuliwapa mtambo maalum wa cherehani iliyowezeshwa umeme wa nishati ya jua kwa ajili ya shughuli za ushonaji nguo mbalimbali hasa maeneo ya vijijini," anasema Swai.

Pia, cherehani imeunganishwa mfumo wa kuchaji simu ili kuwasadia kujiongezea kipato kwa kuchaji simu za wateja, pia simu zao kupata nguvu za kutosha bila ya utegemezi wa umeme wa shirika la Tanesco.

Anasema, kupitia mradi huo fedha wanazozipata kutokana na biashara ya ushonaji nguo na kuchaji simu wanasaidiana pale mmoja wao anapofikwa na tatizo, kama vile msiba, ugonjwa, sherehe, matibabu kulipa ada za shule, chakula na masuala mengine ya kijamii.

**USHONAJI**

Swai anasema, mpaka sasa wateja wao wakubwa ni wanaoishi katika maeneo haujafahamika vizuri katika maeneo mengi ya kata ya Chanika na chama hichi kina

wanachama 35, wakiwamo mafundi cherehani wawili waaliopata mafunzo kutoka taasisi ya Veta.

Anasema kuwa mara nyingi wanapata tenda ya nguo wakati wanafunzi wanapokaribia kufungua shule na katika mfumo wa kuchaji simu, anasema mara nyingi wanapata wateja wakati umeme wa Tanesco unapokatika.

Kwa mujibu wa Swai, kabla ya huduma hizo, walifanya utafiti kwa miezi miwili kubuni mradi sahihiwa kibiashara.

"Katika utafiti huo kwanza tuliangalia vigezo vifuatavyo: kikundi kiwe kimesajiliwa, kikundi kiwe kinajulikana na kiwe chini ya manispaa ya ilala, kiwe kimesajiliwa na kinajulikana kwa mujibu wa sheria, kanuni na kilicho na wanachama walio hai lakini pia wapo tayari kupokea mafunzo kwa ajili ya uendeshaji biashara," anasema.

Katika utafiti huo, walifanikiwa kupata vi-

INAENDELEA UK. 15

# Mradi nishati jua 'unaowatoa' wenye ulemavu shimoni, wakaibukia kwenye ujasiriamali

INATOKA UK. 14

kundi 20, kati yao vitatu ndiyo vilifanikiwa kukidhi vigezo na mradi huu ulitegemea kufanyika kulingana na vigezo vya kikundi waliyokidhi, ikiwamo Ukwacha na sifa kubwa ya kikundi ni wanaopenda kujishughulisha.

Katika makundi ya walemavu anawataja ni wa macho ambao wanaofanya biashara ya kuuuza mkaa na wafumaji.

**MAFANIKO**

Akielezea mafanikio ya mradi katika kijiji cha Kibindu. Swai anasema nishati ya umeme wa jua umebadilisha maisha ya wakazi kijijini, akitumia umeme huo katika nyumba zao, wanachaji simu, kuonyesha mpira, kuanzisha studio ndogo ya kuingiza nyimbo kwenye simu na huduma za 'CD' na wapo wanaouza vinywaji baridi, tofauti na miaka ya nyuma .

Mbali na hilo, anataja ununuzi wa pikipiki, kuanzisha mradi wa umwagiliaji wa kilimo cha kisasa, eneo la Mkuranga na ujenzi wa nyumba za matofali na bati kwa muda mfupi.

"Kwa mfano, Mzee Hugo Ramadhani, huyu ni mwananchi wa kwanza aliyewahamasisha wananchi wa kijiji cha Kibindu kutumia umeme wa nishati ya jua baada ya kuona mafanikio aliyoyapata mzee hugo kwa muda mfupi," anasema Swai.

Kabla ya mradi huo kijiji hapo, ansema wananchi waliishi kwa shida, waliezeka kwa nyasi na taa za vibatari

"Katika kijiji cha Kibindu wanatoza Sh.300 gharama ya kuchaji simu na mwananchi anapata Sh. 540,000 kwa mwezi," anasema

**MLEZI UKWACHA**

Mlezi wa Ukwacha, Said Kwaro, anasema chama cha watu wenye ulemavu kilichoanzishwa mwaka 2004 kwa ajili ya kusaidiana kulingana na changamoto walizo nazo.

"Ni chama kipo katika mtaa wa Lukooni, kata ya Chanika na Kwaro anashukuru kupatiwa cherehani inayotumia umeme wa jua, ili waweze kujiongezea kipato na kupambana na umasikini.

"Hivi sasa kipato chetu kimeongezeka angalau kwa siku tuna uwezo wa kupata Sh. 5000 hadi 7000 kwa siku kwa kushona tofauti na miaka ya nyuma," anasema, huku akidokeza biashara ya kuchaji simu, hivi sasa wanapata Sh.3000 kwa siku na wateja wanaongezeka, umeme wa Tanesco unapokatika.

Anasema, ingawa wafadhili Sepcon wamesaidia kupata cherehani, bado hawana vitendea kazi vya kuuza na malifghafi ya ushonaji kwa hivi sasa anategemea sana wateja wanaokuja kushona viraka tu, ndiyo maana mradi wanashindwa kukua kibiashara.

Hivi sasa wanachama wanawawaomba wafadhili kuwanunulia shamba ili waweze kujikita katika kilimo cha mboga na kununua pikipiki mbalimbali kama Bajaji.

Pia, wana ombi serikalini, iwatengee eneo maalumu ili wajenge nyumba zao na kuacha kuwa tegemezi kwa sababu asilimia kubwa ya walemavu hawana biashara, na wanaishi kwenye nyumba za kupanga.

Pia wanachama wanahitaji mafunzo jinsi ya kutengeneza sabuni, kapeti, mafuta na bidhaa nyingine ili wasiendelee kuwa tegemezi.



Mlezi wa kikundi cha Umoja wa Kusaidiana Walemavu Kata ya Chanika, Said Kwaro, akiwa amekaa katika eneo ilipo ofisi ya chama cha watu wenye ulemavu. **PICHA ZOTE: BERATRICE PHILEMOM.**



Mtafiti wa dawa, katika kiwanda binafsi nchini Ujerumani akifuatilia ubunifu wa kupata dawa ya corona, **PICHA: MTANDAO.**

# Corona na sura tofauti za uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MFALME Salman wa Saudi Arabia, leo ni siku yake kuongoza mkutano wa kilele usio wa kawaida kwa njia ya video na viongozi wa nchi zilizostawi na zinazoinukia kwa kasi kiuchumi - la G20.

Lengo ni kujadili janga la virusi vya corona na kuweka mbinu za pamoja za kupambana nalo duniani, ambalo sasa limegeuka kilio cha dunia, ikigusa mataifa na majina makubwa duniani.

Saudi Arabia, inaesema katika taarifa hiyo, kuwa majadiliano hayo yatalenga kupambana na janga hilo na kuhakikisha uimara wa uchumi duniani.

Viongozi wa mataifa ya Hispania, Jordan, Singapore na Uswisi, watajiunga kwenye mkutano huo pamoja na Umoja wa Mataifa, Benki ya Dunia, Shirika la Afya Duniani (WHO) na wadau wengine.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ametoa wito wa kuanzishwa mfuko mkubwa kutoka G20, utakaosaidia kupambana na janga la virusi vya corona.

Wakati hofu ya janga la ugonjwa corona ikitawala katika sura hiyo, huko Ujerumani katika tasnia ya soka kuna lake katika uchumi na fedha.

Vyombo vya habari na hasa magazeti, vinaripoti namna vilabu vya soka vyenye tamaa ya pesa vimeendekeza kuhakikisha havipotezi mamilioni ya mapato yao, licha ya michezo kusimama kwa muda.

Ilifikia hatua, Waziri wa Afya wa nchi hiyo, Jens Spahn, alilazimika kuingilia kati siku ya Jumapili iliyopita kutamka tena marufuku ya mikusanyiko mikubwa, hapo ikigusa tasnia ya soka na ushabiki wake.

Inalaezwa, hata hivyo vilabu vya Ligi ya Shirikisho la Ujerumani - DFL vina utajiri wa kutosha kuhimili mapumziko ya muda mfupi wa ligi, pasipo kutetereka na nyendo zake.

Hadi sasa nchini humo, juhudi za kutafuta chanjo dhidi ya virusi vya corona zinaendeshwa, matumaini makubwa yakiwa katika kampuni ya dawa ya mjini Tubingen iitwayo CureVac, inayomilikiwa na tajiri Dietmar Hopp.

Mkemia Friedrich von Bohlen, ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya kampuni ya CureVac, anasema kampuni hiyo mbali ya kuwekeza nguvu kutafuta chanjo, wanafanya pia tafiti ya tiba dhidi ya ugonjwa wa corona.

Kwa mujibu wa Bohlen, utafutaji wa chanjo bado ni kipaumbele na kuna mafanikio kadhaa yamekwishapatikana, wakitarajia karibuni wataanza kufanya majaribio ya sampuli kadhaa za chanjo kwenye maabara.

Watu wengi barani Ulaya, taarifa za maendeleo hayo ni muhimu, kanuni za kuwalazimisha watu kujitenga na kuzuia mikusanyiko kutokana na wasiwasi wa kusambaa virusi corona zimeanza kuwachosha wakazi wa bara hilo, hususan msimu wa kiangazi unapokaribia.

Lakini wataalamu wametahadharisha bado ni mapema mno kushusha pumzi. Suala la kutafuta chanjo au tiba linajumuisha masuala mengi, ambayo wakati mwingine ni ngumu kutabiri jinsi yatakavyokwenda.

Ingawa wanasayansi wa Ujerumani, kama Mkemia Bohlen wanaridhishwa na mchango wa serikali kufadhili tafiti za msingi za tiba ya umma, wengi wana fikra kuwa serikali za nchini Ulaya zinaona haja ya msukumo zaidi kwa kampuni binafsi zinazofanya utafiti.

Tafiti na ugunduzi mbalimbali bado zinakwama kufikia matokeo sahihi, kwa sababu watu binafsi hawana mitaji ya kutosha kuendeleza kile walichokigundua.

- **KWA MUJIBU WA TAARIFA ZA KIMATAIFA.**

BIASHARA

MWALONI:

# Soko la kimataifa ufukweni mwa Ziwa Victoria lililosheheni bidhaa sangara

## •Dagaa, 'mapanki' wateja wakuu EAC

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

SAMAKI aina ya Sangara ni maarufu katika ukanda wa Maziwa Makuu nchini na wanapatikana katika Ziwa Victoria pekee,ambako walaji wake wengi ni wa nchini na nchi zingine jirani, kama vile Burundi, Rwanda,Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo(DRC)

Aidha, samaki hao wanavuliwa na kuuzwa zaidi viwandani na mabaki yake yanauzwa katika Soko la Kimataifa Mwaloni, jijini Mwanza.

Iko wazi, mgeni yeyote kutoka nje au ndani ya Tanzania, anapokanyanga ardhi ya jiji la Mwanza ni lazima asikie kuwepo kwa soko hilo maarufu kwa wateja wa Ukanda wa Afrika Mashariki.

Sangara wako tofauti na samaki wengine, kwani ni wakubwa maradufu kuliko samaki wengine walioko katika Ziwa Victoria. Hapo, wanatajwa samaki kama vile sato, nembe, ningu, gogogo, kambale na kamongo.

Ni kawaida mabaki ya sangara yamekuwa yakiuzwa katika soko hilo la Mwaloni, kupitia ushirika wa wachakata samaki aina ya sangara unaoitwa kwa kifupi Uwasa, baada ya samaki hao kukosa sifa ya kusindikwa minofu ya viwandani.

Kimsingi, wateja wake wakuu ni wafanyabiashara hao wa Ushirika wa Wachakataji Samaki Mwaloni, wanaonunua mabaki hayo na kisha wanauza kwa wafanyabiashara kutoka nchi jirani, hasa Burundi na DRC, ambako ndiko kwenye masoko ya walaji wengi zaidi katika nchi jirani.

**UCHAKATAJI WAKE**

Mwenyekiti wa Uwasa, Joshua Kirangi, anaelezea jinsi uchakataji wa mabaki hayo ya sangara wanaoachwa viwandani, kwa kukosa kiwango cha kusindikwa minofu, tayari kwa kusafirishwa kwenda kwenye soko kuu la nchi za Ulaya.

"Huwa tunanunua mabaki ya samaki wanaoachwa viwandani na sisi tunawatengeneza kwa ajili ya kuwauza kwa wafanyabiashara wa Burundi, Rwanda na Congo(DRC), ambao husafirisha kwenda kuuzia nchini mwao," anaeleza Kirangi.

Anasema, samaki hao wanapofika katika soko hilo, jambo walioanza nalo ni kuwaandaa kwa kuwatengeneza na hatua ya pili, ni kuwapasua minofu yao.

Kirangi anataja hatua ya tatu ni kuwawekea ulinzi wa kuwachanganya na chumvi wasiharibike na hata kama wanaweza kukaa wastani wa miezi mitatu hadi sita pasipo kuharibika.

Anasema, hatua ya nne baada ya kuwekwa juani wakauke na wanakamilisha mchakato huo, kwa kuwauza kwa wataja wao tajwa, wakiwa salama wana uwezo wa kudumu kipindi kirefu.

**MAKUNDI YAKE.**

Licha ya uchakataji wa samaki hao kufanyika, pia Kirangi anataja makundi mbalimbali kwa ajili ya kuuzwa sokoni, ikiwamo samaki anauzwa kama alivyo.

Pia, kuna suala la samaki kuundwa kwa kugawanywa katika vikundi maalum,kama vile vichwa, kifua,mifupa, minofu midogo,minofu mikubwa, mikia kwa ajili ya chakula cha kuku, minofu ya chipsi koromeo ambayo, husafirishwa kwenda nchini Uganda kwa ajili ya mboga.

Kiongozi huyo anasema, utaratibu wa sokomi ni kwamba, kila kipande kinauzwa kwa bei yake.

Wasifu mwingine wa bidhaa za sokoni ni kwamba, samaki huyo anatoa mafuta ya kukaangia samaki wengine, ambayo yanasafirishwa kupelekwa katika masoko yaliyoko kwenye mikoa na nchi jirani yanakohitajika.

Mwenyekiti huyo wa wanaushirika wauzaji na wachakataji samaki, anataja wastani wa bei yao hapo sokoni Mwaloni, ni kati ya Sh.8, 000 na Sh. 20,000, katika masoko ya nchi jirani ya Kenya, pia nchini zaidi katika mikoa ya Arusha, Singida na Mbeya

Pia, Kirangi anasema samaki wanatoa mabondo, yanayouzwa zaidi kwa wateja ambao ni jamii ya Wachina, ingawa anakiri katika upande wa pili wa shilingi kwamba hajui hasa wanatumia kwa mahitaji gani. Hiyo inafanya, hakuna kinachotupwa kutokana na bidhaa hiyo ya samaki sangara

Anakiri walakini walio nayo, kwamba hadi sasa hawana vifaa rasmi vya kuwawezesha kutumia katika uchakataji wa samaki hao, kwa ajili ya kuwapelekwa sokoni.

**WACHUUZI WAFUNGUKA**

Sikitu Tizigaranyila, ni mwanamke mchuuzi wa sangara katika soko hilo la Mwaloni, anayetoa picha kamili katika biashara kwa sasa kwamba ni ngumu, tofauti na zamani, kwani anashindwa kumaliza bidhaa anazonunua sokoni.

"Hali ni ngumu mwandishi wa habari (wa Nipashe) Nikinunua mzigo samaki wa Sh.200, 000 tu nauza wanabaki tofauti na hapo nyuma, nilikuwa nauza wanaisha. Naona hali ya uchumi wa soko la sangara imebadilika sana," anasema Sikitu.

Anasema, ni biashara anayoifanya zaidi ya miaka mitatu sasa, lakini bado ni ngumu, akiuza samaki kwa kupanga vipande kulingana na ukubwa wake.

KiongozI wa wauza samaki sokoni hapo, Fikiri Magafu, anaiomba serikali kushusha kodi ya dagaa, kwani imechangia wafanyabiashara kama za Rwanda na DRC, kukimbilia nchi zingine, baada ya kushindwa kumudu ukubwa wa kodi.

Anatoa mfano, kwamba tangu mwezi Julai mwaka jana, serikali ilipandisha kodi ya dagaa kwa kilo, akitaja wastani kati ya Sh. 368 na Sh.460, akifafanua:

"Serikali ilipandisha kodi ya dagaa tangu mwaka jana kusababisha wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kushindwa kumudu na kuacha kuja kununua tena dagaa,hivyo tunaiomba ishushe kodi hiyo ili wafanyabiashara hao warudi kununua."

Magafu anasema, wanunuzi hao wa dagaa kutoka nchi jirani za Burundi,Uganda,Rwanda, Malawi, Zambia na DRC, wamelazimika kuacha kuja kununua dagaa kwenye soko hilo, badala yake anadai wengi sasa wanakimbia soko la Mwaloni, wakihamia Zanzibar, pia katika nchi za Ethiopia, Msumbiji na Kenya.

Analalamika kwamba, ahadi ya kodi katika samaki kuishishwa bado hijatekelezwa na kushuka soko, kumefanya bei ya samaki kushuka kwa gunia kutoka Sh.110,000 hadi Sh,90,000,wakati awali liliuzwa kati ya Sh.160,000 na Sh.180,000.

Kimsingi biashara ya dagaa sokoni hapo haina bei elekezi, bali ni mfumo wa soko huria unaotawala na kuna wakati inapanda na kushuka, kupingana na kiwango cha upatikanaji wake.

Kwa mujibu wa Magafu, soko kuu la dagaa wa Ziwa Victoria, ni katika mikoa ya Arusha, Mbeya Dar- es Salaam, kutokana na wanunuzi wa nje kuacha kuja kufika nchini.

• ***Mwandishi wa makala hii, anapatikana kwa anwani ya barua pepe: anthonygervas@yhaoo.com na simu: (+225) 0682 86 92 44, Kanda ya Ziwa.***



Mabaki ya samaki wa viwandani aina ya sangara yaliyopasuliwa na kuchanganywa na chumvi, katika Soko la Kimataifa la Mwaloni, Mwanza. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

**"Wasifu mwingine wa bidhaa za sokoni ni kwamba, samaki huyo anatoa mafuta ya kukaangia samaki wengine, ambayo yanasafirishwa kupelekwa katika masoko yaliyoko kwenye mikoa na nchi jirani yanakohitajika.**



KiongozI wa wauza samaki sokoni hapo, Fikiri Magafu.

# BIASHARA KATIKA PICHA



Vikundi vya wachimbaji wadogo Wilayani Kishapu, wakifanya maandalizi ya kuchenjua mchanga wa almasi katika eneo lilioko nje kidogo ya mji mdogo wa Maganzo Shinyanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Mchuuzi wa matunda aina ya tende, akisubiri wateja katika eneo la Ilala, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Baadhi ya wananchi wakiingia na kutoka ndani ya Soko Kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, huku kukiwa hakuna vifaa vya kunawa maji au vitakasa mikono (sanitizers), kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

BIASHARA

# UNATAKA KULIMA KITUNGUU MAJI? ELIMU YAKE HII HAPA

Na Mwandishi Wetu


Shamba la vitunguu. PICHA ZOTE: MTANDAO.

VITUNGUU ni zao la pili kutumika kila siku katika mlo wa familia na vinachukua nafasi kubwa katika

matumizi ya mboga, ikiwamo kachumbari na kiungo cha mboga, nyama na samaki.

Majani ya kitunguu hutumika kama mboga kwa baadhi ya jamii, pia inatumika kutengeneza supu.

Katika kilimo chake, kinatoa wastani wa tani 10 hadi 16 Kwa ekari sawa na magunia 80 hadi 160.

Vitunguu ni zao muhimu nchini, hasa katika mikoa ya Arusha, Manyara, Iringa, Mbeya, Tanga, Singida na Kilimanjaro

AINA ZAKE

Aina bora za vitunguu ni pamoja na Mang'ola red, Red creole na Bombay Red. Hizi ni mbegu bora ambazo zinatoa mazao mengi kuanzia kilo 40 hadi 60 kwa hekta, iwapo masharti yakizingatiwa.

Kitunguu kinazalishwa kutokana na mbegu na miche na inakuzwa kwenye kitalu kabla ya kupandikizwa shambani, miche inakuwa na kuzaa vitunguu, ambavyo vikikomaa, vinavunwa na kuhifadhiwa vikiwa katika hali ya kulala bwete.

Wingi na ubora wa vitunguu hutegemea; hali ya hewa, aina ya vitunguu, upatikanaji wa mbegu bora, kilimo bora, uangalifu wakati wa kuvuna, usafirishaji na hifadhi bora.

**HEWA & UDONGO**

Vitunguu hustawi vizuri kwenye maeneo yasiyo na mvua nyingi sana, yana baridi kiasi na kuna wakati yanakuwa na joto.

Upandaji wa mbegu zake nchini kwa ujumla huanza mwezi Machi hadi Mei kutegemea na msimu wa kilimo. Hivyo, kilimo hiki hufanyika mara baada ya mvua za masika kubwa kwisha.

Kipindi cha kiangazi na baridi huruhusu ukuaji mzuri wa vitunguu. Kiasi cha Kilogram 1.5 hadi mbili na mbegu hutosha kwa ekari moja.

Mbegu za vitunguu huoteshwa mapema katika kitalu. Na zinaweza kupandwa kwa mstari au kwa kutawanya katika tuta la kitalu. Katika upandaji wa mstari, mbegu hupandwa katika nafasi ya sentimeta 10 hadi 15 kati ya mstari mmoja na mwingine.

Baada ya kupanda mbegu, hufunikwa kwa udongo na baada ya mbegu kuota, yaondolewe na badala yake kichanja cha nyasi kinajengwa, ili kuiwekea kivuli mimea michanga. Mbegu huota baada ya siku 7 hadi 10.

**UPANDIKIZAJI MICHE**

Upandikizaji mche wa kitunguu bustanini, unafanyika baada ya miche kukua na kufikia ukubwa wa unene wa penseli. Mara nyingi, miche hii itakuwa imesha kaa kitaluni kwa siku 40 baada ya mbegu kupandwa.

Wakati wa kupandikiza miche, haishauriwi kukata wala kupunguza majani. Ipandikizwe katika nafasi ya sentimeta 30 kati ya mstari na mstari na sentimeta 10, kati ya mche na mche.

> **"Dalili za kugundua, pale yaliyo shambuliwa na wadudu hawa huwa na mabaka meupe yenye kung'aa. Katika hali iliyo kithiri majani yote hugeuka kuwa na tabaka nyeupe au kijivu cheupe na baadaye majani hunyauka kabisa.**

Vijaruba vya mraba hutumika kwenye maeneo yenye ardhi tambarare na iliyo kame ili kuhifadhi maji baada ya kumwagilia. Kwa sehemu zenye udongo mzito na zenye maji mengi tumia matuta yenye mwinuko wa semtimta 10 hadi 5 kutoka usawa wa ardhi.

**UMWAGILIAJI**

Kitunguu kinahitaji maji ya kutosha katika kipindi chote cha ukuaji mmea na hasa kutunga kitunguu.

Katika kipindi kisicho na mvua, umwagiliaji ufanyike kila mara ikiwa vilivyopandwa katika vijaruba.

Ili kuharakisha kukomaa kwa vitunguu unashauriwa kupunguza kiasi cha maji ya kumwagilia, taratibu kadri zao linavyo kuwa.


Wakulima wakivuna vitunguu.

Ni siku ya baadaye, 90 hadi 150 kutegemea na aina ya mbegu, kudhibiti magugu

Katika bustani ya vitunguu, magugu yanaweza kutolewa kwa njia ya kutifulia kwa jembe dogo, kung'olea kwa mkono, pia kutumia dawa ya kuua magugu.

Mtu anaondoa magugu kwa kutifulia, epuka kutifua kwa kirefu kutoharibu mizizi na vitunguu vyenyewe, kwani mizizi ya vitunguu, ipo juu juu sana.

**MAGONJWA YAKE**

Viroboto vitunguu; ni wadudu waharibifu namba moja wa zao la vitunguu hapa nchini Tanzania. Husababisha upotevu mkubwa wa mavuno.

Dalili za kugundua, pale yaliyo shambuliwa na wadudu hawa huwa na mabaka meupe yenye kung'aa. Katika hali iliyo kithiri majani yote hugeuka kuwa na tabaka nyeupe au kijivu cheupe na baadaye majani hunyauka kabisa.

Pia, kuna funza, minyoo ya mizizi nao sana tabia ya kukatika miche yao. Hao wanakabiliwa kwa kuzingatia mzunguko wa mazao bustanini.

**MAGONJWA VITUNGUU**

Ukungu mweupe; hujionyesha kipindi cha baridi iliyoambatana na unyevunyevu mwingi hewani.

Dalili za kugundua ugonjwa huo, una rangi ya zambarau katika majani.

Pia, majani hugeuka rangi na kuwa njano na baadaye kunyauka, upenya hadi chini kwenye tunguu na kusababisha kuoza kwake, kwani hakuna dawa ya kuponyesha.

Ukungu wa kahawia; unaweza kuleta madhara makubwa wakati vitunguu vikiwa bustanini na ghalani.

Dalili zake, hujitokeza kwenye majani na baadaye hutoa doa la zambarau. Vikovu hivyo hukua na kutengeneza vidonda kuweka mzunguko katika jani zima au shina la kitunguu.

Baada ya wiki tatu tangu kuingia ugonjwa huo, majani yote huanguka na kukauka.

Ni ugonjwa unaoshambulia vitunguu hata baada ya kuvuna kwa kupitia shingo ya kitunguu au sehemu yoyote yenye kovu, kidonda au mkwaruzo.

Namna ya kuzuia, ni katika bustani, mara uonapo kitunguu chenye dalili za ugonjwa, ondoa mimea na kuiteketeza kwa moto kuzuia au kupunguza kuenea au kinga ya bustani ya dawa.

Tumia kilimo cha kuzungusha au kubadilisha mazao katika eneo la bustani yako. Usipande mfululizo jamii yoyote ya vitunguu katika shamba ulilovuna vitunguu.

Wakati wa kuvuna, epuka kukata au kusababisha vidonda katika vitunguu na baada ya mavuno, anika vitunguu juani kwa siku moja au mbili kabla ya kuviweka katika magunia au ghalani.

Ugonjwa wa kuoza mizizi; unaotoka udongoni na unasababishwa na vimelea vya jamii ya ukungu.

Dalili zake, ni mizizi kugeuka rangi na kuwa njano na baadaye zambarau.

Baada ya muda ugonjwa huenea na mizizi hufa kwa kunyauka.

• ***Kwa mujibu wa taarifa za kitaalamu.***

UCHUMI

# Shirika TIRDO na mipango ya kuinua viwanda vinavyosuasua

**Na Nimi Mweta**

MOJA ya taasisi ambayo imekuwa na kazi nyingi za kufanya katika kipindi kilichopo, kuwajibikia kuinua uchumi wa viwanda, ni Shirika la Utafiti na Uendelezaji wa Viwanda (Tirdo).

Taasisi hiyo iliyopo tangu mwaka 1979, ina jukumu la ama kubuni au kutoa ramani ya mifumo ya teknolojia, huku kukiwapo ziada isiyofahamika kwa wengi, kwamba, kuna suala la kusimamia ubora wa bidhaa na mwelekeo wa masoko, eneo lenye taasisi nyingi zinazoshughulikia.

Dk. Lugano Wilson, ni Mtafiti wa Mifumo ya Kitekonlojia Viwandani, anayeongoza watafiti na wataaluma kwenye taasisi hiyo, kuangalia hali ya kiwanda (hasa vile vya zamani vilivyobinafsishwa halafu vikakwama).

Katika mapitio hayo, ndiyo wanapata picha ya teknolojia iliyopo au iliyokuwepo, namna ya kubadilishwa, gharama husika na bidhaa zinazofaa kuzalishwa kulenga masoko yanayohitajika kwa wakati husika.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipotembelea kiwanda cha nguo Urafiki. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mtafiti huyo anasema, katika upembuzi huo, suala la msingi ni teknolojia na katika mtazamo wa kiuchumi, ni maeneo yanayojitokeza baadaye.

Dk. Lugano anaeleza kwamba, uwezekano wa waliokabidhiwa mwanzo kiwanda kilichodidimia ni mdogo sana, hivyo zaidi ni wawakezaji wapya walio na mipango tofauti ndiyo wanaotafuta ushauri wa kina hasa upande wa teknolojia.

Suala ni kwamba wengi kati ya waliobinafsishiwa awali walikuwa hawajajiandaa kimtaji kumudu kuendesha shughuli hizo, mazingira ambayo hayazungumzii kwa undani.

Anachoelezea ni mabadiliko ya kile kinachohitajiwa katika soko, katika kutengeneza bidhaa na kutazamia kuwa zitapata soko ya zaidi masoko ya nje.

Kimsingi, kuna mahitaji na uangalizi mkubwa zaidi wa kiteknolojia katika miaka ya karibuni, ikilinganishwa na miaka ya 1970 hadi 1980, ambao viwanda vilijengwa au vilikuwa vinafanya kazi, lakini dunia haikufikia mapinduzi makubwa kiteknolojia.

Kwa maana hiyo, hitaji la utafiti au ushauri wa aina ya teknolojia inayofaa kwa mahitaji ya sasa na vifaa, kulinganisha na teknolojia iliyokuwapo awali, ni masuala ambayo watafiti Tirdo kila siku wanakabiliana nayo.

Inaelezwa, kwa sehemu kubwa teknolojia mpya inahitajiwa, isipokuwa katika baadhi ya viwanda vichache ambavyo bidhaa zake hazijabadilika.

Moja ya maeneo ya utafiti ambayo yanaleta changamoto kwa wataalamu Tirdo ni hitaji la kutofautisha teknolojia za viwanda vya ngazi tofauti katika uzalishaji wa bidhaa na upana wa masoko.

Kuna viwanda vidogo ambavyo kiutamaduni, teknolojia yake inapatikana katika Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), ila katika mazingira ya utandawazi kuna kinachoitwa kitalaamu 'app' (application) zinazoweza kutoka popote na kubadili mazingira ya uzalishaji kwa ngazi hiyo.

> **Kuna viwanda vidogo ambavyo kiutamaduni, teknolojia yake inapatikana katika Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), ila katika mazingira ya utandawazi kuna kinachoitwa kitalaamu 'app' (application) zinazoweza kutoka popote na kubadili mazingira ya uzalishaji kwa ngazi hiyo.**

Teknolojia mpya zina tabia ya kupunguza idadi ya wafanyakazi wanaohitajiwa, hali inayoinua kupatikana faida.

Eneo moja linaloonekana kuleta utata katika ushauri wa teknolojia ya kutumia, ni kiwango ambacho kinaweza kutolewa na serikali kuwa viwanda vya ndani vitamudu ushindani dhidi ya bidhaa za kutoka nje.

Dk. Lugano anasisitiza hitaji hilo ni muhimu katika kuendeleza viwanda vilivyobinafsishwa na kukwama, hasa ikizingatiwa nchi za nje zinazalisha bidhaa nyingi kuliko mahitaji yao.

Kutokana na hilo, anasema wazalishaji hao wa kigeni, wanatafuta masoko mengine, ili wauze bidhaa zao kwa 'bei ya kutupwa.'

Watengenezaji wanafidiwa kwa kiasi tu na serikali, kurudisha gharama zao na viwanda vya ndani ya nchi vishindwe kumudu.

Ni hali inayotambuliwa kuwa ni 'ushindani usio haki' na kuna kanuni za biashara ya kimataifa kuzuia hali hiyo, ila si rahisi kwa nchi tofauti kukubaliana wapi kuna msaada kwa kampuni kuhujumu soko la viwanda vya ndani inakopeleka bidhaa zake.

Nchi zinadhibiti hali hiyo kwa kuweka viwango vikubwa vya kodi, dhidi ya bidhaa kutoka nje zinazouzwa kwa bei 'poa' katika soko la nchini.

Wanaohitaji viwanda vilindwe, ni wale walioajiriwa katika viwanda hivyo na wanaoviendesha,wakati walaji kwa jumla wanafurahia bidhaa nzuri tena za bei poa.

Utandawazi kimsingi ni mazingira ambayo vizuizi vya kodi za kuingiza vitu kwa dhamira ya kulinda viwanda vya ndani vinaondolewa, lakini si wataalamu wote wanaoafiki mwelekeo huo, huku Dk. Lugano anasema kulinda viwanda siyo hiari.

Nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) zilikubaliana mwaka 2016, kuwa zingepunguza na kusitisha kabisa uagizaji nguo zilizotumika ndani ya miaka mitatu, ili kutoa nafasi sekta ya viwanda katika eneo hilo kujinasua.

Hata hivyo, alipoingia madarakani nchini Marekani mwanzoni mwa mwaka 2017, Rais Donald Trump kupitia utawala wake, alitoa angalizo kuwa suala hilo linasaidia wasiojiweza wanaosomba nguo kama hizo na wafanyabiashara, kulipia usafirishaji wake na asilimia ndogo tu ya thamani yake.

Licha ya taasisi hizo haziwakilishi maslahi makubwa nchini humo, zina wafuatiliaji wengi wanaochangia nani apigwe kura, tamko hilo likaondolewa ikabaki Rwanda, peke yake kulitekeleza na hivyo ikafutwa katika mpango wa kuingiza bidhaa za Afrika bila ushuru, Agoa.



Ng'ombe akichinjwa katika kiwanda cha nyama, kilichopo Sumbawanga.

UCHUMI



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibasila, wakinolewa kwa mafunzo. **PICHA: MTANDAO**

# Ijue programu inayowafanya vijana kujitambua kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

SUALA la ushauri limekuwa muhimu kwa vijana na kuwapatia matokeo chanya, huku wengine wakifanikiwa kuwa mfano wa kuigwa.

Baada ya kujengewa uwezo wa kufikiri kwa mapana zaidi na hatimaye kufikia ndoto zao na hasa kuwa na maisha bora katika jamii zao.

Hivi karibuni kampuni ya simu iliamua kunufaika kuwekeza katika programu ya ushauri, ikiwa sehemu ya falsafa ya kampuni kuwajengea vijana uwezo na kuwawezesha kutumia fursa zilizopo.

Vijana waliopitia programu ya ushauri wengi, wamefanikiwa na mafanikio ya kujiamini zaidi na kutamani makubwa katika maisha yao ya baadaye.

Mfuko wa kijamii wa Vodacom Tanzania Foundation unaozingatia maendeleo ya kiteknolojia, kwa ajili ya kuboresha maisha ya watu, kwa kushirikiana na wadau wengine nchini unashughulikia

Mwaka 2017 kampuni hiyo kwa kushirikiana na taasisi nyingine, waliendesha programu maalumu iliyolenga kutoa ushauri na kufundisha wanafunzi katika shule za sekondari za Kibasila na Kilangalala, jijini Dar es Salaam.

Ni shirika lisilo la kiserikali lililoko jijini Dar es Salaam linalojihusisha na kuhamasisha vijana na kuwawezesha kujitambua, pamoja na fursa zilizopo kufikia ndoto zao, wachukue hatua ya kuwa wabunifu na kugeuka hachu ya mabadiliko katika jamii zao.

Programu hiyo ililenga kuwasaidia wanafunzi kutengeneza mipango ya maisha yao kwa siku zijazo na ufahamu wa ajira, kisha inawaunganisha na washauri ambao ni wafanyakazi wa kampuni ya Vodacom.

**WASHIRIKI**

Zakia Mrisho (20), ni Mshiriki katika programu hiyo anayedai kuona ndoto zake zinaelekea kutimia, baada ya kushiriki katika programu hiyo, anawahimiza wanafunzi katika shule kadhaa za wilaya ya Kisarawe anakotoka kuhusu umuhimu wa elimu na fursa zilizopo.

Huyo ni mwasisi wa taasisi ya Smart Heroes Foundation, ambayo kazi yake kubwa ni kuwashauri vijana walioacha shule na ana mpango wa kuandaa tovuti yenye taarifa mbalimbali za uelimishaji vijana na hasa wasichana.

Zakia anaeleza kufanikiwa kutafutia wafadhili kwa ajili ya masomo ya stashahada ya teknolojia ya mawasiliano, ajiendeleze.

Albert Chinguile, ni mwanafunzi kijana anayeshiriki katika programu katika Shule ya Sekondari ya Kilangalala, ana ushuhuda wa matokeo chanya ya programu ya ushauri kwa vijana.

Baada ya programu hiyo, Chinguile anasema alijikuta amebadili mwelekeo wake wa kuikusudua kuacha masomo ya sayansi, akiwa mpya anayejiamini katika kupanga malengo yake yajayo.

Kwa sasa, Chinguile ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika stadi ya Saikolojia ya Binadamu, msingi wa kufika hapo ni ushauri awa awali.

'Kupitia programu hiyo maalumu nilipata nafasi ya kufahamiana na watu maarufu na taasisi mbalimbali ikiwamo hii ya Bridge for Change ambapo nafanya kazi kwa sasa," Chinguile anafafanua

> "Programu ilikuwa na manufaa kwani kuna mambo mengi nimejifunza, kwa mfano, namna wanavyofanya uamuzi. Wachache wanaonekana kuwa na dhamira kimaisha huku wengine wakionekana kutokuwa na uhakika wa kile wanachokihitaji katika maisha yao."

**MSHAURI PROGRAMU**

Najenjwa Mbagga, ni mshauri kutoka kampuni ya Vodacom Tanzania, aliyeshiriki katika programu hiyo katika nafasi ya ushauri, anasema ulikuwa wakati mzuri kwake kubadilishana mawazo na wanafunzi, hasa wale wanaosoma sekondari za kata.

"Programu ilikuwa na manufaa kwani kuna mambo mengi nimejifunza, kwa mfano, namna wanavyofanya uamuzi. Wachache wanaonekana kuwa na dhamira kimaisha huku wengine wakionekana kutokuwa na uhakika wa kile wanachokihitaji katika maisha yao."

"Nilitarajia wengi wao kukubali fursa hiyo ya mafunzo. Lakini wengi walionekana kutotambua faida zinazotokana na programu hiyo. Wale ambao walijiunga na programu hiyo na wakaifuatilia kwa karibu wameanza kuchukua hatua ili kufikia ndoto zao," anasema Mbagga.

Mbagga anaelezea kuwa kila mmoja bila kujali taaluma yake, anahitaji mshauri na kuna umuhimu wa mpango wa ushauri kuanzia ngazi ya darasa la kwanza.

"Kwa mtindo huu, watoto wetu watakuwa na ufahamu ambao wanaupata katika hatua ya awali. Elimu yetu inaweza kusonga mbele zaidi kuliko mtu yeyote anavyotarajia," anasema.

> "Ndiyo maana kuwa na mshauri ni jambo la muhimu sana ili kuondoa hali ya vijana kufanya mambo bila kufikiri kwa undani, lakini pia kutengeneza fursa zenye mafanikio."

Happiness Shuma, ni mshauri mwingine anakotoka Mbagga, anasisitiza umuhimu wa ushauri kwa ajili ya kujenga maarifa na stadi kutoka kwa mshauri kwenda kwa mshauriwa.

Anaendelea: "Nilipata taarifa mbalimbali na maarifa na kufahamu suala zima la uhitaji wa ushauri katika jamii," alisema.

**WARATIBU PROGRAMU**

Ochek Msuva, Ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Bridge for Change, anasema ushirikiano wake na kampuni hiyo ya simu, umechangia kwa kiasi kikubwa kuwafikia vijana 18,000 kwa kutoa mafunzo kwa vijana 600 ndani ya miaka mitatu iliyopita.

"Mpango huu ulitoa mchango mkubwa sana, kwa sababu mara nyingi vijana wako hatarini kufanya uamuzi usiokuwa sahihi,: anasema Msuya na kuongeza:

"Ndiyo maana kuwa na mshauri ni jambo la muhimu sana ili kuondoa hali ya vijana kufanya mambo bila kufikiri kwa undani, lakini pia kutengeneza fursa zenye mafanikio."

Msuva, anaeleza kampuni anayotumikia ilihudumia mahitaji yote ya programu hiyo, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wake kushiriki katika kufundisha na kuwashauri wanafunzi.

Pia, mradi mwingine wa 'Together with Vodacom Tanzania Foundation' ambao kwa kiasi kikubwa ulionyesha mafanikio ya kujenga maabara tatu za kisayansi katika shule tatu tofauti.





Mafundi bomba wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), wakitengeneza bomba lililokuwa limepasuka katika eneo la Sokoine jijini Mbeya juzi, ikiwa ni moja ya mikakati ya mamlaka hiyo kudhibiti upotevu wa maji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vijiji vyahadharishwa ugawaji ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

VIONGOZI wa vijiji wameshauriwa kufuata taratibu za kisheria katika kugawa ardhi ya vijiji kwa wawekezaji.

Miongoni mwa mambo ya kuzingatia ni kuwashirikisha wananchi badala ya kujiamulia wenyewe ili kuepuka kuibua migogoro kati ya wananchi na wawekezaji.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Ofisa Mipango Miji kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Enock Kyando, alipokuwa anatoa elimu ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya Uturo, Mtamba, Ukwama na Kapunga wilayani Mbarali.

Kando ambaye ni Mjumbe wa Kamati Maalumu ya Uelimishaji wananchi kuhusu umuhimu wa uhifadhi na ujirani mwema, alisema, mkutano mkuu wa kijiji ndio wenye mamlaka ya kugawa ardhi ya kijiji. Alisema kazi ya viongozi wa vijiji hasa ofisa mtendaji na mwenyekiti ni kupokea maombi ya wanaotaka kupewa ardhi na kuitisha mikutano ya vijiji, ili wananchi wajadili na kuridhia ama kutoridhia kugawa ardhi yao kulingana na uhitaji.

"Msimamizi mkuu wa ardhi ya kijiji ni wanakijiji wenyewe, na ndio wanaotakiwa kuamua kumpa mtu mwingine ardhi yao kwa ajili ya matumizi ambayo wataona wao inafaa, kiongozi ukifanya maamuzi mwenyewe unasababisha migogoro," alisema Kyando.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya ardhi, kijiji kinaruhusiwa kugawa ardhi isiyozidi hekta 50 kwa mtu mwingine na kwamba ikizidi ukubwa huo zipo mamlaka zingine ambazo zinahusika na hivyo mhitaji wa ardhi hiyo atatakiwa kuziona. Kuhusu mpango wa matumizi bora ya ardhi, Kando alisema kila kijiji kinatakiwa kuwa na matumizi bora ya ardhi kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasaidia kuondoa migogoro ya ardhi kwa kuepusha mwingiliano wa shughuli za kibinadamu.

Alisema katika kipindi hiki ardhi ni muhimu na inahitaji usimamizi wa karibu, na kwamba bila hivyo kuna hatari ya kutokea vita ya wenyewe kwa wenyewe.

Vilevile, aliwashauri wananchi kumiliki ardhi yao kisheria kwa kuyatafutia hati miliki ili kuwa na uhalali wa kuitumia kama dhamana wakati wanapokopa fedha kwenye taasisi za kifedha.

Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Mbarali, George Mwaijobelo, alisema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na migogoro mingi ya ardhi kutokana na vijiji vingi kutokuwa na matumizi bora ya ardhi.

Alisema kutokana na elimu ambayo kamati yao inaitoa kwa wananchi baadhi ya vijiji vimeanza kuwa na uelewa na kwamba vijiji hivyo vimeanza kupanga matumizi bora ya ardhi.

"Ardhi yetu haiongezeki lakini binadamu tunaongezeka na mifugo yetu inaongezeka, kwa hiyo ni lazima tuwe na matumizi bora ya ardhi kulingana na shughuli zetu za kiuchumi na kijamii," alisema Mwaijobelo.

Alisema baadhi ya maeneo yanatakiwa kutengwa kwa ajili ya kilimo, makazi, kuchungia mifugo na shughuli zingine za kijamii ikiwamo maeneo ya viwanda na taasisi za Serikali.

Baadhi ya wananchi wa vijiji hivyo waliishukuru Serikali kwa kuanzisha utaratibu huo, wakisema kuwa utawasaidia kumaliza migogoro ya ardhi ambayo walidai imezidi katika wilaya hiyo.

# DC atoa elimu ya corona sokoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KUTOKANA na tishio la virusi hatari vya Covid -19 vinavyosababisha ugonjwa wa corona, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ameanza kuingia kwenye masoko mbalimbali ya Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi.

Ntinika alianza utaratibu huo juzi, ambapo amekuwa akiwaelimisha wananchi mbinu mbalimbali za kujikinga na janga hilo ikiwemo kuepuka kusalimiana mikononi na kukumbatiana.

Akizungumza katika Soko la Sido jijini Mbeya, aliwataka wananchi wote wa Jiji la Mbeya kuhakikisha wananawa mara kwa mara mikono kwa kutumia maji yanayotiririka na sabuni.

Alisema wakazi wa Mkoa wa Mbeya wana utamaduni wa kusalimiana mikononi na kukumbatiana, hali ambayo alisema ni hatari kutokana na tishio la ugonjwa huo.

"Ugonjwa huo haujaingia mkoani kwetu lakini kinga ni bora kuliko tiba, hivyo nawaomba epukeni sana huu ugonjwa, fuateni maelekezo ya wataalamu wa afya yanayotolewa kila siku, humu kwenye masoko ni hatari kwa sababu bado kuna mikusanyiko," alisema Ntinika.

Alisema zoezi la kutoa elimu ya ugonjwa huo litakuwa endelevu hasa kwenye maeneo yenye mkusanyiko wa watu kwa maelezo kuwa walianza kwenye magari ya abiria na sasa wanaendelea kwenye masoko. Aliwataka wananchi kupuuza michezo inayofanywa na baadhi ya watu wanaoigiza kuhusu ugonjwa huo pamoja na kutoa taarifa za upotoshaji ambazo zinawafanya baadhi ya watu kuacha kuchukua tahadhari.

Baadhi ya wafanyabiashara walisema pamoja na elimu wanayopatiwa, lakini kuna tatizo kwenye bidhaa wanazonunua wakidai kuwa zinashikwashikwa na watu wengi wakati wa kununua.

Mmoja wa wafanyabiashara wa nguo za mitumba katika Soko la Sido, John Mtalike, alisema wateja huwa wananunua nguo hizo kwa kuchagua na kuzirudisha ambazo hawana mpango wa kuzinunua lakini wengine wanakuja wananunua na kuondoka nazo.

"Kinachotufanya tuendelee kuuza ni dhiki tu ya maisha, vinginevyo tulitakiwa tufunge biashara zote kama ambavyo nchi zingine zilivyofanya maana tunaweza kuambukizana kupitia bidhaa zetu," alisema Mtalike.

# Sababu mrundikano wa kesi kupungua

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

KAIMU Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Mbeya, Lugano Mwakilasa, amesema kuwa hali ya mrundikano wa kesi imepungua kwa kiasi kikubwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa mujibu wa Lugano, hali hiyo imetokana na uwapo wa usimamizi thabiti wa mwenendo wa kesi hizo.

Kauli hiyo alitoa jana wakati akizungumza na Nipashe na kubainisha kuwa kupungua kwa mashauri hayo ya kesi kunatokana na ushirikiano mzuri wa kushughulikia kesi hizo uliopo kati ya wapelelezi wa kesi hizo, waendesha mashtaka na mkemia mkuu wa serikali kwa mkoa wa Mbeya.

Alisema kwa sasa wanakesi chache, ambazo hazizidi 16 ambazo zinatakiwa kujadiliwa na kuwa hali ya kusikilizwa kwa kesi mbalimbali inaendelea vizuri kutokana na jitihada za makusudi zinazoendelea kufanywa na mahakama hiyo katika kupunguza mrundikano.

Alisema ofisi ya mwanasheria wa serikali inawajibu wa kuwasimamia wapelelezi wa kesi mbalimbali, pamoja na waendesha mashtaka kwa lengo la kuhakikisha upelelezi unakamilika kwa wakati kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo za kimahakama.

"Unajua ofisi ya mwanasheria wa serikali ina wajibu na nguvu ya kuwasimamia wapelelezi na waendesha mashtaka kwa lengo la kuhakikisha upepelezi unakamilika kwa wakati ili shauri liweze kusikilizwa kwa muda mwafaka," alisema Lugano.

Alisema ofisi ya mwanasheria wa serikali ina nguvu na mamlaka ya kuhakikisha kuwa kesi mbalimbali zinakamilika kwa muda unaotakiwa ili kuepukana na mrundikano wa kesi bila ya sababu za msingi.

Pia Kaimu huyo Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Mbeya alisema uwiano wa kusikilizwa kwa mashauri wa hapo awali ni tofauti na sasa kwa kuwa kuna mabadiliko ya mambo mengi ya kimahakama ambayo yameweza kufanyika kwa lengo la kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani.

Alisema kwa sasa hakuna tabia ya maahirisho ya mashauri bila sababu za msingi kwa kuwa mfumo wa sasa, unawataka wapelelezi wa kesi mbalimbali kuwasilisha ushahidi uliojitosheleza dhidi ya washukiwa wa kesi hizo ikilinganishwa na hapo zamani na ambapo kesi nyingi zilikuwa zikiahirishwa mara kwa mara kutokana na kutokidhi ushahidi.





# Waziri aagiza kufanyike ukaguzi shule ya Bunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA MJINI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ameagiza watendaji wake kuanza ukaguzi wa shule maalum ya wasichana inayojengwa na Bunge, ili kutoa ushauri utakaosaidia usajili kufanyika kwa wakati.

Vilevile, ameahidi kuunga mkono juhudi za wabunge katika ujenzi wa shule hiyo inayojengwa katika Kata ya Kikombo jijini Dodoma.

Prof. Ndalichako alitoa agizo hilo jana alipotembelea shule hiyo akiwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, ili kujionea maendeleo ya ujenzi wake.

Katika ziara hiyo, waziri huyo aliwaagiza Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, na Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule, Euphrasia Buchuma, kuanza hatua za ukaguzi wa shule hiyo ili usajili ufanyike kwa wakati pindi itakapokuwa imekamilika. Alisema wizara itatoa mchango katika kuunga mkono ujenzi wa shule hiyo kwa kuwa ni alama kubwa itakayoachwa na Bunge la 11 linaloongozwa na Spika Ndugai.

"Nimefarijika sana na kazi hii yenye ubora wa hali ya juu na nitaongea na wenzangu wizarani ili tuone namna nzuri ya kutoa mchango wetu ili kuunga mkono kazi hii kubwa inayofanywa na Bunge," aliahidi.

Alisema mchango wao utaangalia namna ya kuongeza majengo kutokana na ukubwa wa eneo inakojengwa.

"Natumaini tukiongeza majengo hayo, itaongeza idadi ya wanafunzi watakaokuwa wanadahiliwa katika shule hii," alisema.

Prof. Ndalichako alifurahishwa namna Bunge hilo lilivyoamua kujenga shule kwa ajili ya wanafunzi wa kike ili wapate fursa ya elimu.

Spika Ndugai alisema wabunge wa Bunge la 11 wamejitolea kuchangia ujenzi wa shule hiyo pamoja na kufanya shughuli mbalimbali za kuhamasisha uchangiaji ili kutimiza lengo hilo.

Kiongozi huyo wa Bunge, alisema shule hiyo itakuwa na miundombinu yote na imezingatia viwango na mwongozo wa serikali.

"Shule hii inatarajiwa kuchukua wanafunzi 320 wa kidato cha tano na sita na ina miundombinu yote ikiwamo madarasa, maabara, mabweni, bwalo la kisasa la chakula, vyoo vya mfano, ofisi za walimu, jengo la utawala, maktaba yenye miundombinu ya Tehama na chumba cha afya," alisema.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati), akiongozana na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (kulia), alipotembelea na kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Bunge ya kidato cha tano na sita iliyopo Kikombo wilayani Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Machinga watakiwa kuondoka barabarani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imewataka wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, wanaofanya biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi ikiwamo barabarani, kuondoka kwa kuwa ni maeneo hatari kiusalama na kiafya.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alipozungumza na viongozi wa wafanyabiashara hao kuhusiana na kampeni endelevu ya kuwaondoa wale wote wanaopanga biashara zao katika maeneo yasiyo rasmi.

Alisema maeneo kama barabara za magari na watembea kwa miguu, darajani na mitaroni ni hatari kwao na wateja, hivyo wafanye biashara kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya biashara hizo badala ya kuvamia maeneo yasiyo rasmi kwao.

Aliwataka viongozi wao kushirikiana na jiji kutoa elimu, ili kuondoa tatizo la kufanya biashara bila mpangilio wowote.

"Wengi wao wamepanga biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi kama vile mitaro ya maji, madarajani na barabarani, ninachowaambia Halmashauri ya Jiji kamwe haitakubali kuona sheria na kanuni zinapuuzwa, ni muhimu wakajiondoa wenyewe kabla mali zao hazijaharibiwa na kusababisha hasara kubwa kwao," aliagiza.

Ofisa huyo pia aliwataka wafanyabiashara kufanya biashara kwenye masoko yaliyoko karibu kwenye kata zote kwa kuwa nafasi bado zinapatikana.

Katibu wa wafanyabiashara hao, Victar Sijila, alisema kuwa na vitambulisho vya machinga isiwe sababu ya kukiuka sheria na kanuni zilizowekwa na halmashauri kwa kufanya biashara bila mpangilio.

Alisema viongozi wanaunga mkono operesheni ya kuwaondoa wale wote wanaokiuka sheria na kanuni kwa kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Katibu huyo alisema kuwa baadhi ya wafanyabiashara hao wamepanga bidhaa zao kwenye maeneo hatarishi na hakuna sababu ya kukaidi kuondolewa kwenye maeneo hayo ambayo si rasmi kwao kufanyia biashara.

Mweka Hazina wa Wafanyabiashara hao, Enjoy Mlemwa, aliwataka wamachinga kuwa waadilifu katika kazi kwa kuheshimu mipaka ya maeneo wanayofanyia biashara.

# Akumbusha watendaji alichoagiza Rais JPM

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, ameitaka menejimenti ya wizara hiyo kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia weledi katika kutekeleza maagizo ya Rais John Magufuli ya kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa chakula.

Alitoa rai hiyo katika hafla ya makabidhiano rasmi ya ofisi na aliyekuwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mathew Mtigumwe, yaliyofanyika makao makuu ya wizara, Mtumba jijini Dodoma.

Kusaya alisema Wizara ya Kilimo inatakiwa kuhakikisha Watanzania wanakuwa na uhakika wa chakula kwa kuzalisha mazao kwa wingi na kwa ubora.

"Kila mtumishi wa Wizara ya Kilimo ahakikishe anafanya kazi kwa bidii na weledi kutekeleza malengo yote tuliyowekewa na Rais John Magufuli kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika na usalama wa chakula," alisema.

Kusaya alimshukuru Mtigumwe kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa Wizara ya Kilimo wakati wa uongozi wake ikiwamo kupitia mabadiliko yaliyofanyika katika idara na taasisi.

Mtigumwe alisema anawashukuru watumishi wote wa wizara hiyo kwa ushirikiano waliompa alipokuwa Katibu Mkuu na anajisikia vyema kuona wizara na taasisi zake wanachapa kazi.

Alisema kero za sekta ya ushirika na umwagiliaji zinahitaji msukumo mkubwa kuzitatua ili taswira ya Wizara ya Kilimo iendelee kuwa nzuri.

"Ushirika bado ni tatizo, nawaachia japo tulianza mchakato wa maboresho ya sheria endeleeni ili wakulima wa Tanzania wanufaike na jasho lao," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi, Mkurugenzi wa Mipango Bora ya Ardhi ya Kilimo, Paulo Tarimo, alimshukuru Katibu Mkuu aliyepita, Mtigumwe, kwa ushirikiano na maelekezo aliyoyatoa wakati wa utumishi wake.

Mkurugenzi huyo aliahidi kwa niaba ya menejimenti na watumishi wa wizara ya kilimo kutoa ushirikiano zaidi kwa Katibu Mkuu Kusaya, ili malengo ya taifa yafikiwe.



## Bosi wizara awapa neno watahiniwa

**Na Mwandishi Wetu,** UNGUJA

WANAFUNZI wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kidato cha sita, nne na pili mwaka huu, wametakiwa kutumia dharura ya kufungwa kwa shule kujisomea vizuri wakiwa nyumbani.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Asiya Iddi Issa, alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema hakuna shaka kwamba mitihani itafanyika, lakini itategemea hali ya maendeleo ya ugonjwa wa corona.

Alisema kipindi hiki ambacho shule zote zimefungwa, ni wakati mwafaka kwa wanafunzi hao kujisomea majumbani na kubadilishana maarifa katika masomo yao ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mitihani ya taifa.

Alisema huu si wakati wa kupoteza kwa wanafunzi bali ni fursa nyingine ya kujisomea kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo ya mitandao.

"Wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kitaifa jaribuni kutumia muda huu kujiandaa zaidi kwa ajili ya mitihani yenu kusoma kwa njia mbalimbali ikiwamo mitandaoni," alisema. Mkurugenzi huyo alisema siri ya kufaulu katika mitihani ni kusoma na kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya mitihani husika.

Alisema wanafunzi wanayo fursa nyingine ya kujisomea na kupitia mitihani mbalimbali iliyopita ya Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) ambayo inapatikana katika mitandao.

"Zipo njia na mbinu mbalimbali ambazo wanafunzi wanaweza kuzitumia katika kipindi hiki ambacho shule zimefungwa ikiwa ni sehemu ya matayarisho ya mitihani ya taifa," alisema.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, aliwataka walimu kuongeza juhudi ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo inayotazamiwa kufanyika mwaka huu.

"Shule zimefungwa lakini masomo yanaendelea na zipo njia na mbinu mbalimbali za kujisomea ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mitihani ya taifa," alisema.

# Shein aonya ukaidi corona

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wananchi kuacha ukaidi na kufuata maelekezo ya serikali kukabiliana na virusi vya corona.

Dk. Shein alisema hayo alipotembelea eneo linalotarajiwa kujengwa jengo la uchunguzi wa maradhi makuu katika Taasisi ya Utafiti wa Afya, Binguni wilayani Kati Unguja.

Alisema katika kukabiliana na virusi vya ugonjwa huo, serikali tayari imetowa maelekezo kadhaa ili kujikinga na virusi hivyo, akiwataka wananchi kuacha ukaidi na kutekeleza maelekezo ya kudumisha usafi kama inavyoelekezwa.

Alisema virusi vya ugonjwa wa corona ni janga la kimataifa na ni maradhi yasiotaka mzaha na hayachagui aina ya mtu, hivyo ni vyema wananchi wakaondokana na ukaidi na kuzingatia maelekezo ya serikali.

Rais Shein alisema serikali imeingia katika vita dhidi ya adui asiyeonekana na ikalazimika kuchukua hatua mbalimbali za dharura ikiwamo kuzuia makongamano na kuzifunga shule zote na wanafunzi kukosa taaluma.

Alisema serikali haiwezi kuainisha ukubwa wa gharama inazopoteza kutokana na hatua ilizochukua katika kukabiliana na virusi vya corona, sambamba na athari za kiuchumi zitokanazo na kuvurugika kwa sekta ya utalii, ambayo huchangia asilimia 80 ya fedha za kigeni.

Rais Shein pia aliwataka wananchi kuachana na upotoshaji kupitia mitandao ya kijamii.

Alisema serikali itakamilisha miradi yote ya maendeleo iliyoanzishwa, ikiwamo ya ujenzi wa nyumba Kwahani, Michenzani Mall, barabara, Mahakama Kuu na mingineyo.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, alisema wizara yake imejiandaa kikamilifu kushirikiana na Serikali ya Watu wa China katika dhana ya kukuza utaalamu ili kuleta ufanisi wa maabara itakayojengwa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akibadilishana mawazo na Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, wakati alipofanya ziara ya kuangalia ujenzi wa maabara ya uchunguzi na utafiti wa virusi katika eneo la Binguni, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mahakama Kuu yasitisha shughuli mwezi mmoja

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

MAKAHAMA Kuu Zanzibar, imesitisha usikilizaji wa kesi zote kwa muda wa siku 30 kuanzia jana hadi Aprili 24 mwaka huu, ikiwa ni tahadhari ya kujikinga na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar, Muhamed Ali Muhamed, alisema kesi ambazo ziko katika hatua ya kusikilizwa, mahakama itawaruhusu mawakili au wenye kesi kuwasilisha kwa maandishi.

Alisema mahakama zitashughulikia kesi za dharura na kwa washtakiwa wenye kesi nzito na maombi ya dhamana, mwombaji na wakili wake au kwa ombi la dhamana, wadhamini ndiyo watakaoruhusiwa kuingia mahakamani.

Mrajis huyo alisema kwa makosa yenye dhamana, majaji na mahakimu wanatakiwa kutoa dhamana yenye masharti nafuu ili kupunguza mrundikano katika magereza kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa huo.

"Katika kipindi hiki watendaji wote wa mahakama wataendelea kuwapo kazini. Hata hivyo, kumbi za mahakama (open court) hazitatumika," alifafanua.

Alisema majaji na mahakimu wenye hukumu na uamuzi, watatumia kipindi cha sasa kuzikamilisha.

"Zaidi ya mwongozo uliotolewa, sanitizers na hatua nyingine za kinga zinawekwa mahakamani hapa," alisema.

# Serikali yamwaga maelfu vitabu shuleni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, imepokea na kugawa vitabu vya masomo mbalimbali vikiwamo vya masomo ya sayansi vya mtaala mpya katika shule za msingi 72.

Vitabu hivyo zaidi ya 22,553 vimegawiwa ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa shule hizo.

Vitabu hivyo vimetolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, huku zaidi ya vitabu hivyo 20,188 vikiwa vya darasa la sita na miongozo kwa walimu.

Awali walimu walikuwa wakiandaa masomo kwa kutumia vitabu vilivyopo kwenye mitandao.

Akigawa vitabu hivyo, Ofisa Elimu (Vifaa na Takwimu) wa shule za msingi katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, Sadick Juma, alisema kila mwanafunzi atapatiwa kitabu na atakayepoteza, mzazi au mlezi atawajibika kukilipa au kukirejesha kabla ya muhula haujamalizika.

Aidha, alisema wamegawa vitabu vya mtaala mpya vya masomo ya Kiswahili, Hisabati, Sayansi na Teknolojia, Maarifa ya Jamii, Uraia na Maadili na vya lugha ya Kiingereza, na kwamba kila somo ni vitabu 2,884 kwa darasa la sita pekee sawa na vitabu 20,188.

Pia, alisema kwa darasa la awali wamegawa vitabu 242 kwa kila somo la Hisabati, Kuandika, Kusoma, Michezo na Sanaa, huku darasa la pili wamegawa vitabu 223 vya masomo ya Afya na Mazingira, Hisabati, Kuandika, Kusoma na Michezo na Sanaa.

"Kama mwanafunzi anaweza kutunza daftari la darasa la kwanza mpaka anafika darasa la saba bado anakuwa nalo, basi akipatiwa kitabu hiki ataweza kukitunza...kwa mwanafunzi atakayepoteza kitabu hiki, mzazi wake au mlezi atawajibika kukilipa," alisema Juma.

Aliongeza: "Lengo la kugawa vitabu hivi kwenye shule zetu za msingi zote 72 ni kuhakikisha vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi na vitabu vya miongozo kwa walimu zinapatikana na kuwapunguzia gharama walimu kuandaa masomo kwa njia ya mitandao."

Akizungumza kwa niaba ya walimu wakuu, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Malunga, Beatrice Katama, alisema kuwa vitabu hivyo vitasaidia kuondoa changamoto ya ukosefu wa vitabu vya masomo ya sayansi vya mtaala mpya hasa kwa darasa la sita, awali na darasa la pili.

# Mama asakwa tuhuma kumtupa mtoto chooni

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linamsaka mwanamke asiyefahamika kwa tuhuma za kujifungua watoto mapacha kisha kumtumbukiza chooni mmoja wao na kutokomea kusikojulikana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, tukio hilo lilitokea Machi 22 majira ya asubuhi katika Kijiji cha Namlangwa, Kata ya Lyowa, Tarafa ya Matai Wilaya ya Kalambo.

Alisema kuwa siku hiyo mwanamke aliyefahamika kwa jina la Venerenda Maembe (65) aligundua kuwa kuna mtoto mchanga ametupwa ndani ya shimo la choo chake na mtu asiyefahamika.

Baada ya kubaini hilo, aliomba msaada kwa majirani na walipofika walifanya jitihada za kubomoa choo hicho na kufanikiwa kumtoa mtoto huyo, lakini alikuwa ameshafariki dunia kutokana na kushindwa kupata msaada wa haraka.

Hata hivyo, kamanda huyo alisema hakuna mtu aliyekamatwa kutokana na tukio hilo, lakini kuna mwanamke aliyekuwa amejifungua watoto mapacha kijijini hapo siku chache kabla ya tukio hilo.

Alisema walipomfuata alipokuwa akiishi karibu na tukio hilo, walikuta nyumba yake mlango uko wazi bila yeye kuwapo. Kamanda Masejo alisema baada ya kuingia ndani ya nyumba hiyo walikuta mwanamke huyo ameshahama kwenye nyumba aliyokuwa amepanga bila kuwaaga majirani.

Kutokana na kitendo hicho, alisema Jeshi la Polisi linahisi kuwa ndiye aliyehusika kumtupa mmoja kati ya watoto hao akihofia ugumu wa maisha na namna ya kuwalea.

Alisema polisi wanaendelea kumsaka mwanamke huyo na atakapokamatwa, atafikishwa mahakamani.



Baadhi ya walimu wakuu wa shule za msingi za Halmashauri ya Mji wa Kahama, wakichukua vitabu vya mtaala mpya kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la sita, awali na darasa la pili vya masomo mbalimbali katika halmashauri hiyo, mkoani Shinyanga juzi, vilivyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TPSF yapongezwa angalizo ajira

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI kadhaa nchini wamepongeza angalizo lililotolewa na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) kwa waajiri kuwa maambukizi na kuenea kwa corona lisichukuliwe kama kisingizio cha kuwapunguza wafanyakazi kiholela.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wafanyakazi wengi wamepongeza hatua ya taasisi hiyo kutoa angalizo mapema kabla ya kuenea maambukizi mengi kwani waajiri wengi wasiowaaminifu hupenda kutumia majanga kupunguza wafanyakazi kama hatua ya kupambana na athari za kutokea janga.

"Kama mfanyakazi nimefarijika sana na tamko au angalizo la TPSF na kuungwa mkono na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kuwa wapo waajiri wengi katika sekta binafsi watakaotumia corona kama sababu ya kupunguza au kubana maslahi ya wafanyakazi," alisema Seif Almas, mfanyakazi wa kiwanda wa kimoja cha kutengeneza mifuko mbadala jijini Dar es Salaam jana.=

Neema Joram wa kiwanda cha kutengeneza vifaa vya ujenzi eneo la Mikocheni, alisema angalizo limetolewa wakati muafaka, huku serikali ikiendelea kutoa mwongozo wa kujikinga na hatua mbalimbali zinazochukuliwa kukabiliana na maambukizi kuenea nchini.

"Angalizo la TPSF kwa waajiri siyo kwamba linaleta ahueni kwa wafanyakazi tu bali hata nchi kwa ujumla ambayo imekuwa ikipata kodi kupitia mishahara ya wafanyakazi, viwanda, mashirika na taasisi mbalimbali," alisema Neema na kuwataka Watanzania kufanyakazi kwa bidii na kuzingatia kinga dhidi ya maambukizi.

Hivi karibuni, TPSF iliandaa mkutano na vyombo vya habari kuelezea dhamira yake ya dhati kuunga mkono na kuipongeza serikali kwa hatua na mikakati madhubuti iliyochukua mpaka sasa kukabiliana na maambukizi ya corona.

Mkutano huo ambao uliongozwa na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Angelina Ngalula, aliwaonya waajiri nchini kuchukua tahadhari ya maambukizi ya corona na kwamba kusiwe na visingizio vya kupunguza wafanyakazi kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo sehemu mbalimbali duniani.

Alisema TPSF imeunda kamati maalumu kushughulikia suala la corona ambapo imejielekeza zaidi katika mambo makuu matatu ikiwapo kutoa elimu ya kutosha kwa jamii kwa mujibu wa muongozo na maelekezo ya serikali kupitia Wizara ya Afya.

HABARI KIMATAIFA

# Ofisa FBI afariki dunia akiwa jela

**TEHRAN, Iran**

OFISA wa Shirika la Ujasusi la Marekani (FBI), Robert Levinson, ambaye alitoweka katika mazingira ya kutatanisha mwaka 2007 nchini Iran, amefariki dunia akiwa kizuizini nchini humo familia yake imesema.

Rais wa Marekani, Donald Trump hajathibitisha rasmi kifo chake, lakini alisema kuwa inawezekana kuwa amefariki dunia.

"Hawajatueleza kuhusiana na kifo chake, lakini watu wengi wanaamini kuwa taarifa hiyo ni sahihi, ni jambo la kusikitisha, inatia huzuni, alikuwa mgonjwa kwa miaka kadhaa," alisema Rais Trump huku akikiri kwamba alishindwa kumrudisha nchini Marekani.

Rais Trump alisema hivi majuzi alipokea habari kutoka kwa maofisa wa Marekani ambao walikuwa wasimamizi wake kwamba Robert Levinson, amefariki dunia akiwa kizuizini baada ya kuzuiliwa kwa miaka kadhaa na mamlaka nchini Iran.

Hata hivyo haikutolewa sababu au tarehe ya kifo cha Levinson, lakini familia yake imebaini kuwa kifo chake kilitokea kabla ya janga la ugonjwa wa virusi vya corona.

**RFI**

**"Hawajatueleza kuhusiana na kifo chake, lakini watu wengi wanaamini kuwa taarifa hiyo ni sahihi, ni jambo la kusikitisha, inatia huzuni, alikuwa mgonjwa kwa miaka kadhaa," alisema Rais Trump huku akikiri kwamba alishindwa kumrudisha nchini Marekani.**

# Wafungwa 4,000 waachiwa huru kuepuka maambukizi ya corona

**ADDISABABA, Ethiopia**

ZAIDI ya wafungwa 4,000 wameachiwa huru nchini Ethiopia ikiwa ni hatua ambayo serikali imechukua ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Mwanasheria Mkuu wa Ethiopia, Getachew alisema Jumatano kuwa wafungwa wote walioadhibiwa kwa kesi ndogo na wanawake ambao wana watoto ndiyo watakaoachiwa huru.

Getachew alieleza kuwa wageni ambao walishtakiwa kwa makosa ya usafirishaji haramu na dawa za kulevya wataachiwa huru pia na kurudishwa katika nchi zao.

Miongoni mwa walioachiwa huru ni mhariri wa habari na mwandishi wa jarida, Fekadu Mahtemework wa nchi hiyo ambaye alirejea nchini Ethiopia baada ya Waziri Mkuu, Ahmed Abiy kuingia madarakani mwaka 2018 wakati ambao maelfu ya wanasiasa waliachiwa huru na hali ya taifa kuwa kwenye dharura kusitishwa huku vyama vya kisiasa vikivunjwa.

Lakini mwandishi huyo alibaki na mashtaka ya kukwepa kodi hivyo kuadhibiwa kifungo cha miaka saba tangu Oktoba mwaka jana.

Hatua nyingine ambazo Ethiopia imezichukua kukabiliana na maambukizi ya corona ni wafanyakazi wengi kufanya kazi nyumbani pamoja na kufunga mipaka yake yote.

Abiria wote wanaowasili Ethiopia wanapaswa kukaa karantini kwa muda wa siku 14 katika hoteli ambazo zimechaguliwa na mamlaka.

Raia wa Ethiopia ambao watashindwa kulipia gharama za karantini, serikali imesema itagharamia.

Zaidi ya wasafiri 400 wameanza kukaa katika karantini kwa lazima, kwa mujibu wa Wizara ya Afya nchini humo. Taifa hilo limefunga kumbi zote za starehe za usiku. Mpaka sasa Ethiopia ina wagonjwa 12 wa Covid-19.

***BBC***




Mmoja wa wananchi wa Afrika Kusini akinunua mahitaji ya bidhaa kwa wingi katika moja ya maduka makubwa ikiwa ni hofu ya ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

# Mawaziri wakuu wastaafu wahukumiwa jela miaka 27

**ALGIERS, Algeria**

MAHAKAMA ya Rufani ya Algeria imewahukumu mawaziri wakuu wastaafu wa nchi hiyo, Abelmalek Sellal na Ahmed Ouyahia kwenda jela miaka 27 kwa makosa ya ufisadi.

Watuhumiwa hao wanashtumiwa kuhusika katika kashfa ya magari na ufadhili haramu wa kampeni ya mwisho ya aliyekuwa Rais wa Algeria, Abdelaziz Bouteflika, kama walivyofanya viongozi wengine wakubwa 20.

Lakini adhabu za baadhi ya viongozi hao zimepunguzwa.

Abelmalek Sellal alihukumiwa miaka 15 na Ahmed Ouyahia alihukumiwa miaka 12, lakini washtakiwa wengine wenye ushawishi mkubwa wakati huo wamejikuta adhabu zao zikipunguzwa.

Hukumu ya kifungo cha miaka 10 katika mahakama ya mwanzo iliyotolewa dhidi ya mawaziri wawili wa zamani wa viwanda imepunguzwa.

Hukumu ya Rais wa zamani wa shirika kubwa la waajiri nchini Algeria, Ali Haddad, imepunguzwa kutoka miaka saba hadi minne.

Kwa jumla, ni karibu viongozi wa zamani wa kisiasa, matajiri wakubwa wenye ushawishi na maofisa wakuu kuhukumiwa na Mahakama ya Rufani tangu mwanzoni mwa mwezi huu.

Wanatuhumiwa kufadhili kampeni ya uchaguzi kwa muhula wa tano wa Abdelaziz Bouteflika mwaka 2019, na ubadhirifu katika sekta ya viwanda na magari.

Hata hivyo, mahakama hiyo imewapa siku nne za kukata rufani kwenye Mahakama ya Juu zaidi nchini humo.

***RFI***

# Aliyekiuka amri ya kukaa nyumbani aliwa na mamba

**KIGALI, Rwanda**

MWANAUME mmoja nchini Rwanda ambaye alikiuka amri ya kukaa nyumbani ambayo inaendelea kutekelezwa nchini humo na kuamua kwenda kuvua samaki ameuawa na mamba.

Taarifa iliyotolewa na Meya wa Wilaya ya Kamonyi ilimtaja mtu huyo kuwa ni Alice Kayitesi na kwamba tukio hilo lilitokea Jumatano asubuhi katika mto Nyabarongo.

"Alikuwa amekiuka sheria ya kukaa nyumbani, alikuwa ni miongoni mwa watu wachache hapa ambao hawaonyeshi ushirikiano katika sheria hii ya kukaa nyumbani ili kuzuwia kusambaa kwa ugonjwa wa virusi vya corona," alisema Kayitesi.

Serikali ya Rwanda iliweka amri ya kukaa nyumbani kwa wananchi wake Jumapili kutokana na kuendelea kuongezeka kwa kasi ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Rwanda imethibitisha kuwa na watu 40 walioathirika na maambukizi ya ugonjwa huo, idadi hiyo ikiwa ni ya juu zaidi kuliko mataifa mengine ya Afrika Mashariki.

Kufungwa kwa shughuli za kiuchumi katika nchi hiyo kumewaathiri watu wengi wenye kipato cha chini.

Serikali imesema kuwa itawasaidia wale wanaohangaika wakati wa hatua kali za kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo.

Wakati huohuo, idadi kubwa ya polisi wamesambazwa katika maeneo mbalimbali ya Rwanda ili kuhakikisha watu wanatekeleza amri ya kukaa nyumbani, kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona.

Wale ambao wametajwa kuwa ni wafanyakazi muhimu, kama vile madaktari na wauguzi, wafanyakazi wa maduka ya jumla na waandishi wa habari, wanaruhusiwa kutoka nyumbani.

Jumatatu, polisi walimpiga risasi na kumuua mwanaume mmoja maeneo ya Jiji la Kigali ambaye walisema alikiuka amri ya kukaa nyumbani.

Polisi walisema kuwa alikua anajaribu kupigana na maofisa wa Jeshi la Polisi.

Kumekua na ripoti za wafanyakazi wanaotembeza bidhaa zao mtaani ambao kwa sasa hawana kipato wanaojaribu kutoroka kutoka mji mkuu Kigali kujiunga na familia zao zilizoko vijijini, wanaotembea mwendo mrefu kutokana na kupigwa marufuku kwa usafiri wa umma.

***BBC***




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi (kulia), akikabidhi sehemu ya mifuko ya saruji tani 10, kwa Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Bugando, Profesa Abeli Mkubi, jijini Mwanza jana, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa wodi ya wagonjwa wa saratani hospitali hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahukumiwa faini mil. 230/-, kifungo cha nje

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewahukumu wafanyabiashara wawili kutumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja na kulipa faini ya Sh. milioni 230 baada ya kukiri kosa la kukutwa na mazao ya misitu aina ya magogo.

Kadhalika, Mahakama hiyo imetaifisha magogo hayo yenye thamani ya Sh. milioni 505.1 kuwa mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliyokutwa nayo washtakiwa hao, Manish Khattar na Rajesh Velram.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Mahakama hiyo iliyoketi bandari kavu ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) Ubungo jijini Dar es Salaam chini Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega.

Hakimu alisema washtakiwa wametiwa hatiani kwa kosa la kupatikana magogo ambayo ni mazao ya misitu isivyo halali.

Alisema kufuatia kosa hilo, anawahukumu kila mmoja kulipa faini ya Sh. milioni 115 na kutumikia kifungo cha nje cha miezi 12 kwa kutotakiwa kufanya kosa lolote la jinai katika kipindi hicho.

Washitakiwa hao wanadaiwa kati ya Januari 15, 2015 na Oktoba 31, mwaka huu, katika eneo la NASACO, Ilala jijini Dar es Salaam, kwa pamoja walikutwa na magogo hayo bila kuwa na kibali kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Hata hivyo, washtakiwa hao walilipa faini hiyo baada ya kufikia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), Biswalo Mganga, ambapo awali walikuwa wakikabiliwa na mashtaka saba.

Washtakiwa hao baada ya kufanya mazungumzo na DPP, walifutiwa mashtaka sita yakiwamo ya kuongoza genge la uhalifu, kughushi, kutakatisha fedha na kukwepa kodi kisha kubakiwa na shtaka moja la kupatikana na mazao ya misitu aina ya magogo.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, upande wa utetezi uliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu nafuu kwa washtakiwa kwa madai wana familia zinazowategemea, ni wakosaji wa mara ya kwanza na wamekiri makosa yao bila kiisumbua mahakama.

**Hukumu hiyo ilisomwa jana na Mahakama hiyo iliyoketi bandari kavu ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) Ubungo jijini Dar es Salaam chini Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega.**

# Afungwa miaka 15 jela udhalilishaji kingono

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma imemhukumu mwanaume wa miaka 23 kwenda jela miaka 15, fidia ya Sh. 500,000 na viboko vitatu baada ya kukiri kosa la udhalilishaji wa kingono dhidi ya binti mwenye umri wa miaka 16 anayefanya kazi za ndani.

Kesi ya udhalilishaji wa kingono namba 31 ya mwaka 2020 inayomkabili Mohamed Athumani, imesikilizwa kwa mara ya kwanza katika mahakama hiyo. Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Benedict Kivuma, mbele ya Hakimu Mfawidhi wa mahakama hiyo, Kenneth Mutembei, alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Januari 7, mwaka huu katika eneo la Mji Mwema.

Kivuma alidai, kwa mujibu wa maelezo ya aliyetendewa kosa, mshtakiwa alikuwa akimtaka kimapenzi kwa muda bila mafanikio na siku ya tukio akiwa ameagizwa dukani alimvuta kwa nguvu na kumpeleka kwenye chumba cha mlinzi karibu na alipokuwa akipita, kisha kumwingizia vidole sehemu za siri kinyume cha sheria.

Hakimu alipomuuliza mshtakiwa kama ni kweli alitenda kosa hilo, naye akakiri mbele ya mahakama hiyo kuwa alitenda tukio hilo na kuomba kusamehewa.

"Ni kweli nilitenda tukio hilo naomba kusamehewa kwa kuwa ni kosa langu la kwanza na pia ninategemewa na mke, watoto na wazazi wangu," alisema.

Baada ya utetezi huo Wakili wa Serikali Benedict Kivuma, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa wote wanaofanya vitendo vya udhalilishaji wa kingono.

Hakimu Mutembei alisema adhabu ya kosa hilo ni miaka 15 hadi 20 ila kwa kuwa hajaisumbua mahakama hiyo kwa kukubali kosa baada ya kufikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza, anamhukumu miaka 15 jela, fidia ya Sh. 500,000 na viboko vitatu.

# Makada CCM kikaangoni Mara

**Na Ambrose Wantaigwa, MUSOMA**

TAKRIBANI miezi saba kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu, Kamati ya Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Mara imewahoji makada wake kadhaa kwa tuhuma za kukiuka taratibu za uchaguzi.

Miongoni mwa wanaodaiwa kuhojiwa ni Naibu Waziri wa Tamisemi, Mwita Waitara, ambaye ameshaonyesha nia ya kugombea ubunge Tarime Vijijini.

Hata hivyo hakuna taarifa rasmi iliyotolewa kwa waandishi wa habari

siku ya juzi kuhusu adhabu wala uamuzi uliofikiwa katika kikao hicho kilichofanyika katika ofisi zake mjini Musoma.

Awali viongozi wa CCM ngazi ya mkoa walieleza kwamba Waitara alikuwa akikabiliwa na tuhuma mbalimbali zikiwamo za kuanza kampeni kabla ya wakati kinyume cha utaratibu, tuhuma ambazo hata hivyo, amekuwa akizikanusha mara kwa mara.

Wengine ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Serengeti, Jacob Bega na Katibu wake, ambao hata hivyo, tuhuma dhidi yao hazikufahamika mara moja.

"Ni kweli niliitwa na Kamati ya Maadili Musoma na kuhojiwa, hii ni

hatua ya kwanza kuna hatua nyingine na siwezi kuweka wazi mambo ya

ndani ya chama kwa kuwa kuna utaratibu wa kutoa taarifa kwa vyombo vya habari," alisema Bega kwa njia ya simu.

Kwa upande wake Waitara anadai safari zake nchi nzima ukiwamo mkoa wa Mara zinatokana na nafasi yake ya naibu waziri kutekeleza majukumu yake ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuhimiza utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM. Waitara aligombea jimbo la Tarime 2010 kupitia Chadema na kupoteza

kwa Nyambari Nyangwine wa CCM. Hata hivyo, alifanikiwa kushinda

Jimbo la Ukonga 2015 kupitia Chadema kabla ya kuhamia CCM na kushinda tena jimbo hilo mwaka jana katika uchaguzi mdogo.


Land Form No. 54 A

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE LAND ACT, 1999
(No. 4 of 1999)
DEFAULT NOTICE
(Under Section 127)

Title No 78378,
Plot No 96,
Block D,
Shariff Shamba Area,
Ilala Municipal,
Dar Es Salaam.

To: FRANK MICHAEL MREMA,
P O BOX 70036,
Dar Es Salaam.
(The Mortgagor)

That be notified of the default to honor your obligations, covenanted under the mortgage with Maendeleo Bank PLC, whereby you have guaranteed **NEW PAN GENERAL TRADING CO.** who have failed to repay the loan facilities on due dates to the extent that, as of March 19th, 2020 the outstanding balance is **Tzs 107,540,281.44**

You are hereby required to pay the said **Tzs 107,540,281.44** so as to rectify the said default. Please be informed that penalties and interest accrues daily

Be further notified that in the event you do not rectify the default stated above within Sixty (60) days from receipt of this notice, we may exercise our right to sell the mortgaged property/land cited above, or appoint a receiver, or lease the property, or enter possession or sue you in court.

Dated at Dar Es Salaam this 19th day of March 2020.

**FOR MAENDELEO BANK PLC**
**(THE MORTGAGEE)**
Served upon me at Dar es Salaam this……day of……………………2020
……………………………………
**Signature of borrower/Spouse/local authority/Guarantor**

MAENDELEO BANK PLC. P.O. Box 216, DAR ES SALAAM 19 MAR 2020 MANAGER

**CC; LILIAN LAWRENCE SHAYO T/A NEW PAN GENERAL TRADING CO.**

215682902

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

---

**Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania**
**Baraza LA ardhi Nyumba Wilaya ya Morogoro.**
**Maombi na.116 ya mwaka 2018.**
**CRDB BANK PLC........MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**MSAFIRI MACHUZA SINGILA.........**
**MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA MSAFIRI MACHUZA SINGILA.**

Popote ulipo unaarifiwa ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 29/04/2020.Wewe mwenyewe binafsi au mtume mwakilishi wako bila kukosa ambapo MAOMBI yamepangwa kutajwa.

Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu Leo tarehe 25 mwezi 03 mwaka 2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

156817

---

**GO PAMOJA COMPANY LIMITED**
**REGISTRATION NUMBER: 141025236**
**P.O.BOX 71995 DAR ES SALAAM**

**NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP VOLUNTARILY**

Pursuant to section 334(1) of the Companies Act Cap 212(2002) we hereby GIVE NOTICE to the public that on 23rd March 2020 the members of GOPAMOJA COMPANY LIMITED resolved to wind up the company voluntarily pursuant to section 333(1)(b) of the Companies Act.

.............................................
NEEMA SHUKURU MOHAMED
FOR AND ON BEHALF OF GOPAMOJA COMPANY LIMITED P.O.BOX 71995,
DAR ES SALAAM
BOARD CHAIRPERSON

156821

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ZAWADI ELLY MGENI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 954 AQJ** yenye chasis namba **FK337D55072** injini namba **60167660202.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TaarifayaPolisi: **IR/TR/RB/880/2020.**

215682502

---

## KUPOTEA KWA KADI

**Mwanaisha Amani Mndeme** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA ISIS yenye usajili wa namba **T 976 DEY** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa : **DAR/KIJ/RB/266727/2020**

115682202

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# BAYERN, DORTMUND KUKATWA MISHAHARA KISA VIRUSI CORONA

**MUNICH, Ujerumani**

WACHEZAJI na Wakurugenzi wa Bayern Munich na Borussia Dortmund wamekubali kukatwa mishahara yao kwa muda kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wamebainisha kwamba uamuzi huo ni kwa ajili ya kuwasaidia kifedha waajiriwa wengine kwenye klabu hizo wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona.

Wachezaji wa klabu ya Union Berlin, inayoshika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Bundesliga, wametangaza kwamba wanamaliza msimu wote bila kulipwa mishahara.

Wiki iliyopita wachezaji wa Borussia Monchengladbach walikuwa wa kwanza nchini humo kukubali kukatwa mishahara yao.

Wachezaji wa Bayern watakatwa asilimia 20 ya mishahara yao, huku wale wa Dortmund watatoa kiasi cha fedha kutoka kwenye mishahara yao.

Hakukuwa na shughuli yoyote kwenye Bundesliga tangu Machi 8, mwaka huu, baada ya mlipuko wa vizuri vya corona kusababisha matukio mengi ya kimichezo kusimamishwa duniani kote.

Wachezaji wote wa kikosi cha kwanza cha Union Berlin wameamua kumaliza msimu huo bila mishahara kwa sababu ya kipindi hiki kigumu.

Wiki iliyopita mshambuliaji wa Bayern, Robert Lewandowski na mke wake Anna walichangia kiasi cha euro milioni 1 kwa ajili ya kusaidia janga hilo.



# TREZEGUET AWANIWA BESIKTAS

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Aston Villa, Trezeguet anawaniwa na Besiktas ikiwa ni mwaka mmoja tu tangu atue pale kwenye dimba la Villa Park.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri alifunga bao ambao liliwapeleka Villa kwenye fainali ya kombe la Carabao, wakati wakishinda kwa uwiano wa 3-2 kwenye nusu fainali dhidi ya Leicester, na ameonekana kuwa na kiwango cha kuvutia kwa kikosi hicho kilichopo chini ya kocha, Dean Smith. Villa walifungwa na Manchester City kwenye fainali ya Corabao.

Trezeguet mwenye umri wa miaka 25, alisajiliwa kipindi cha majira ya joto kutoka kwa klabu nyingine ya Ligi Kuu ya Uturuki, Kasimpasa kwa ada ya pauni milioni 10.

Kama ilivyokuwa kwa wachezaji wengine, Trezeguet hakuwa na uzoefu na soka la Uingereza na alianza kwa kusuasua kabla ya kuanza kurudi kwenye kiwango.

Katika mechi 31 alizocheza Trezeguet kwenye mashindano yote amefunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho tatu.

Kwenye Ligi ya Uturuki, alifunga mabao 25 katika mechi 71 alizocheza na kutoa pasi za mwisho 18.

# Pedro hafikirii majaliwa yake

**LONDON, England**

PEDRO anaweza kumaliza mkataba wake hivi karibuni pale Chelsea, lakini mshindi huyo wa kombe la Dunia amesisitiza "hafikirii" kuhusu majaliwa yake ya baadaye.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alitua pale kwenye dimba la Stamford Bridge mwaka 2015, na amecheza mechi tisa tu za Ligi kuu msimu huu na atakuwa mchezaji huru miezi mine ijayo.

Hata hivyo, kusimamishwa kwa ligi hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, inamaana kwamba bado majaliwa yake hayajajulikana hadi kumalizika kwa msimu wa 2019-20.

Hilo likiwa akilini, Pedro amebainisha kwamba majaliwa yake baadaye hayaisumbui akili yake.

"Namaliza mkataba wangu, lakini sio jambo la muhimu sana kwangu, na nimeacha kufikiria kuhusu hilo," alisema Pedro akiiambia Cadena Ser.

"Kuanzia hapo, kinachofuata kuhusu majaliwa yangu kitakuja tu, lakini kwa sasa sio jambo la muhimu kwangu."



HABARI MICHEZO



# UNITED

## YAONGOZA MBIO USAJILI SANCHO

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United 'inaongoza mbio za kumsajili Jadon Sancho kwa pauni milioni 120' kipindi cha majira ya joto.

Winga huyo wa Borussia Dortmund kwa kiasi kikubwa anatarajiwa kuondoka kwenye ligi hiyo ya Ujerumani, Bundesliga, kipindi cha majira joto huku klabu kadhaa kubwa zikiwania saini yake.

Kwa mujibu wa gazeti la Mirror, United wanaongoza na wapo tayari kutoa pauni milioni 120 kwa ajili ya kuipata saini ya Muingereza huyo.

Sancho alijiunga na Dortmund kutoka kwa mahasimu wa United, Manchester City mwaka 2017.

Liverpool, Chelsea, Barcelona na Juventus ni miongoni mwa klabu zilizoonesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo.

Lakini kiasi cha pauni milioni 120 kinatajwa kama kikubwa, lakini United inaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumsajili.

United inaamini kwamba, kiasi cha pauni milioni 120 kinawakilisha thamani halisi ya Sancho hasa kutokana na umri wake.

Miamba hao wa dimba la Old Trafford pia walijaribu kumsajili Sancho mwenye umri wa miaka 20 kipindi kilichopita cha majira ya joto.

Sancho amefunga mabao 16 katika mashindano yote msimu huu kabla ya ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# Barca kutoa watano kumpata Martinez

**MILAN, Italia**

BARCELONA ipo tayari kutoa ofa ya wachezaji watano kwa ajili ya kufanikisha usajili wa mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez, kwa mujibu wa taarifa kutoka nchini Italia.

Miamba hao wa Katalunya wanaangalia uwezekano wa kuwaachia nyota kadhaa ili kupunguza bajeti kubwa ya mshahara, hasa kutokana hali ya kifedha ya sasa baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

Na kwa mujibu wa gazeti la Corriere dello Sport, Barcelona wataangalia uwezekano wa kuwaachia Arturo Vidal, Arthur Melo, Jean-Clair Tobido, Carles Alena na Nelson Semedo kwenye Inter ili kumpata Martinez.

Barca imekuwa ikihuishwa na mpango wa kumsajili Martinez katika miezi ya hivi karibuni na ndiye mtu anayeonekana kuja kuwa mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez.

Ripoti ya hivi karibuni inaonesha kwamba, mshambuliaji huyo wa Argentina tayari amekubali mkataba wa fedha nyingi pale Nou Camp, lakini bado wanatakiwa kukubaliana kwanza na miamba hao wa San Siro.

Inter ipo tayari kumuuza mchezaji huyo na ipo tayari kukataa kama ada haijafikia kiasi cha pauni milioni 103 ambacho kipo kwenye kifungu cha kuondoka katika mkataba wake.



# Arsenal sasa yapania kumbakisha Ceballos

**LONDON, England**

ARSENAL 'inajiamini' kwamba inaweza kumbakisha nyota wa Real Madrid, Dani Ceballos anayecheza hapo kwa mkopo na kuendelea kucheza kwenye Ligi Kuu ya England.

Mlipuko wa virusi vya corona umefanya ligi nyingi za Ulaya kusimamishwa angalau hadi Aprili 30 ambapo mkataba wa mkopo wa Ceballos unatarajiwa kumalizika Juni 30.

Kwa mujibu wa gazeti la Evening Standard, wakati wa mazungumzo rasmi bado hayajafanywa kati ya Arsenal na klabu yake ya Real Madrid, timu hiyo kutoka London Kaskazini inajiamini kwamba itaweza kuongeza muda wa kucheza na kubakia hapo.

Arsenal bado imebakiwa na mechi 10 za kucheza ili msimu huu umalizike na kusimamishwa kwa ligi huyo hakujatoa hatima kama itaendelea au la baada ya Aprili.


Inatarajiwa kwamba, ligi hiyo itakaporejea itacheza bila mashabiki huku milango ya viwanja ikiwa imefungwa.

Kama Arsenal itashindwa kufikia makubaliano hadi Juni 30 mwaka huu, watakuwa na nafasi ndogo ya kumbakisha mchezaji huyo kwenye kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao.

Mapema Februari mwaka huu gazeti la Marca lilimnukuu Ceballos mwenye umri wa miaka 23 akisema: "Arsenal ilichukua nafasi ya kunisajili mimi na nataka kucheza kwa bidii na kubadilisha mambo hapa."

Arsenal ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa imepitwa pointi nane na Chelsea waliopo nafsi ya nne.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAZARD: NIHUKUMUNI MSIMU UJAO MADRID

●●●Nitahukumiwa katika msimu wangu wa pili, nimekutana na watu wengi wapya…

**MADRID, Hispania**

EDEN Hazard anaamini ingekuwa sahihi kuhukumu wakati wake hapo Real Madrid mwishoni mwa msimu ujao.

Kiungo mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alikubali kujiunga na miamba hiyo ya Hispania Juni mwaka jana, baada ya miaka saba ya mafanikio pale Chelsea, na katika kipindi hicho alitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mara mbili, Europa League mara mbili na kutangazwa Mchezaji Bora wa Kulipwa wa mwaka.

Hata hivyo, akitafsiri mafanikio hayo kwa klabu yake mpya imeonekana kuwa changamoto kwa Hazard, ambaye amefunga mara moja tu katika mechi zake 10 LaLiga alizocheza kabla ya kukumbwa na majeraha ya kifundo cha mguu mwezi uliopita ambayo yana uwezekano wa kumweka nje ya uwanja kwa kipindi chote kilichobaki cha msimu.

Hazard, ambaye alikuwa nje ya uwanja kati ya Novemba na Januari kwa tatizo kama hilo, alikiri umekuwa msimu wa kwanza kwake wa kukumbukwa na Los Blancos, kwa kutambua ana muda wa kushinda kukosolewa huko kunakomzunguka.

"Msimu wangu wa kwanza Madrid umekuwa mbaya, lakini si wote mbaya, ni msimu wa kuzoea," alielezea katika mahojiano na RTBF.

"Nitahukumiwa katika msimu wangu wa pili. Ni kundi kubwa la wachezaji, nimekutana na watu wengi wapya. Umekuwa uzoefu mzuri kwangu.

"Bado nimebakiza miaka minne katika mkataba wangu na ninatumai kuwa kwenye kiwango."

Ingawa alikuwa na nyuzi katika kifundo chake cha mguu ambazo ziliondolewa wiki iliyopita baada ya kufanyiwa upasuaji huko Dallas, Hazard alitarajiwa kuwamo katika kikosi cha Ubelgiji kitakachoshiriki Euro 2020.

Hata hivyo, michuano hiyo imesogezwa mbele kwa miezi 12 kutokana na janga la kimataifa la virusi vya corona.

"Nilitarajia kuwa fiti [kwa michuano ya Euro] hivyo inakatisha tamaa kwamba imeahirishwa," Hazard aliongeza.

"Nilipanga kucheza, upasuaji ulikuwa wiki chache zilizopita sasa.

"Sote tutakuwa na umri wa miaka mwaka 2021, ambayo ni aibu, lakini iniruhusu kuwa katika kiwango.

"Nadhani labda ni ngumu kwa mashabiki kwa sababu wanataka kutazama mashindano ya kimataifa kila msimu wa majira ya joto, kwa hivyo ni ngumu kwao.

"Lakini nafikiria kuwa kuna vipaumbele maishani ambavyo inamaanisha kufutwa. Wanasoka ni kama kila mtu mwishoni mwa siku. Itasubiri hadi mwaka ujao."

## KWA UFUPI

**UPAMECANO ANUKIA ARSENAL**

Arsenal inaweza kuwa njiani kumnasa Dayot Upamecano kutoka RB Leipzig wakati huu beki huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 21, akiwa tayari kuihama klabu hiyo majira ya joto. ***(Bild, via Star)***

**ADEBAYOR AKWAMA BENIN**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal na Tottenham, Emmanuel Adebayor, 36, amekwama Benin kwa sababu ya virusi vya corona. Aliondoka Paraguay, anapoichezea Olimpia, kwa lengo la kujiunga na familia yake nchini Togo, lakini kusimamishwa huko Benin inamaanisha kuwa lazima ajitenge kwa muda wa siku 15. ***(Talksport)***

**CORONA YAICHELEWESHA CHELSEA**

Chelsea imesimamisha mazungumzo ya mikataba mipya kwa wachezaji wake kutokana na janga la virusi vya corona. 'Blues' ina wachezaji wanne ambao mikataba yao inamalizika mwishoni mwa msimu - Kiungo Mbrazil Willian, 31, mshambuliaji Mfaransa Olivier Giroud, 33, winga Mhispania Pedro, 32, na kipa Muargentina Willy Caballero, 38. ***(Telegraph)***

**MISHAHARA BARCA KUFYEKWA 70%**

Barcelona wanataka kuweka punguzo la mishahara kwa wachezaji hadi asilimia 70 kwa muda mrefu kwa kipindi hiki janga la virusi vya corona likiendelea kuitesa Hispania. ***(Guardian)***

**IBRA, CAVANI WATAJWA LEEDS**

MMILIKI wa Leeds United, Andrea Radrizzani ameweka wazi kuwa alijaribu kuwasajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Uruguay, Edinson Cavani, 33, na Msweden Zlatan Ibrahimovic, 38, ambaye kwa sasa yupo AC Milan, katika dirisha la Januari. ***(Mail)***

**UNITED KASI KWA SANCHO**

Manchester United inaongoza mbio za kumsajili mshambuliaji wa England, Jadon Sancho, 20, kutoka Borussia Dortmund wakati dirisha la usajili litakapofunguliwa tena majira ya joto. ***(Independent)***

**MADRID KWA AUBAMEYANG**

Real Madrid inatumai pesa taslimu pamoja na mchezaji zinatosha kuiwezesha kufanikisha mpango wa Arsenal kuachana na mshambuliaji wao, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30. ***(Star)***

**VERTONGHEN NJIA PANDA SPURS**

BEKI wa Tottenham na Ubelgiji Jan Vertonghen, 32, amekiri hana uhakika endapo anataka kusaini mkataba mpya na kubaki Spurs kwa msimu ujao. ***(Mirror)***

**ARSENAL YANOGEWA NA CEBALLOS**

Arsenal inaamini watakuwa tayari kukubali dili na Real Madrid la kuongeza mkataba na kiungo Mhispania Dani Ceballos, 23, baada ya mkataba wake wa mkopo kumalizika Juni 30. ***(Standard)***

**SMALLING KUMPISHA KOULIBALY**

Manchester United ipo tayari kumruhusu beki wa England, Chris Smalling, 30, kuubadili mkataba wake wa mkopo na Roma kuwa wa kudumu, kwa kuzingatia wanaweza kumsajili beki wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly, 28. ***(La Gazzetta dello Sport, via Mail)***

**CASTAGNE AHUSISHWA LEICESTER**

Leicester City imekuwa ikihusishwa na kutaka kumsajili beki wa Atalanta na Ubelgiji, Timothy Castagne, 24. ***(Sport Foot, via Leicester Mercury)***

# RAIS TFF AONGOZA MAMIA DAR KUMZIKA ASHA MUHAJI

**Na Saada Akida**

WADAU wa soka nchini jana walijitokeza kwa wingi katika maziko ya aliyekuwa mwandishi mkongwe wa habari za michezo nchini, Asha Muhaji, ambaye alizikwa katika makaburi ya Mwinyimkuu yaliyopo Magomeni, jijini Dar es Salaam.

Katika mazishi hayo yaliyoanzia nyumbani kwao maeneo ya Kijitonyama kabla ya mwili kwenda kupumzishwa makaburi ya Mwinyimkuu, yalihudhuriwa na watu wengi maarufu wakiwamo viongozi wa klabu kongwe nchini, Simba na Yanga na Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia pamoja na Katibu Mkuu, Wilfred Kidao.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Hajji Manara, alijumuika katika msiba huo na kutoa pole kwa wafiwa huku akiwataka kuwa wavumilivu na wenye nguvu katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na mpendwa wao, Asha.



"Kwa niaba ya uongozi wa klabu ya Simba inayoongozwa na Mtendaji Mkuu, Senzo Mazingisa, tunawapa pole familia ya Asha Muhaji, tunatambua mchango wake katika tasnia ya habari hasa upande wa michezo.

"Asha pia ndiye mwanamke wa kwanza Afrika Mashariki na Kati kuwa ofisa habari wa klabu kubwa," alisema Manara akimzungumzia marehemu ambaye enzi za uhai wake aliwahi kuwa msemaji wa klabu ya Simba.

Asha ambaye alizaliwa mwaka 1974, alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Hindu Mandal jijini Dar es Salaam alipokuwa amelazwa kwa siku chache kwa ajili ya matibabu kabla ya mauti kumfika.

Enzi za uhai wake, Asha aliwahi kulitumikia Shirika la Posta nchini, kisha magazeti ya Majira na Spoti Starehe mwanzoni mwa miaka ya 1990 kabla ya kuhamia Uhuru na Mzalendo na baadaye Bingwa, Dimba, Mtanzania na Rai, huku kwa upande wa Msemaji wa Klabu ya Simba, akiifanya kazi hiyo kipindi cha uongozi wa Alhaj Ismail Aden Rage, mwaka 2014.

Lakini pia Asha atakumbukwa kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha hivi karibuni baada ya kuwa miongoni mwa kundi la waandishi wa habari la kuhamasisha ushindi kwa timu ya Taifa, Taifa Stars. Pumzika kwa amani Asha Muhaji, umekamilisha safari yako ya duniani. Mungu ailaze roho yako mahali pema peponi. Amen.

## Mkude, Chama watajwa viungo bora

**Na Saada Akida**

HUKU Ligi Kuu ikiwa imesimama kutokana na kuepuka kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), kiungo wa Yanga, Papy Tshishimbi na wa Azam FC, Salum Abubakari 'Sure Boy', wametaja nyota wao wawili waliowavutia katika idara hiyo hadi ligi inapigwa 'stop' na serikali.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alipiga marufuku ya mikusanyiko yote isiyo ya lazima, ikiwamo shughuli zote za michezo kwa kipindi cha mwezi mmoja kutokana na virusi vya corona kutangazwa kuwa janga la kimataifa.

Hata hivyo, Tshishimbi na Sure Boy wakizungumza na mwandishi wetu kwa nyakati tofauti wiki hii, alipowataka kwa mtazamo wao kutaja wachezaji waliong'ara katika idara yao hadi ligi hiyo inasimama, hawakusita kumtaja viungo wa Simba, Jonas Mkude na Clatous Chama. Tshishimbi alisema Mkude ni mchezaji mzuri na kwamba ni miongoni mwa viungo ambao anawakubali na kutamani kucheza naye timu mmoja.

"Mkude ni mchezaji nzuri sana, ana kipaji pia anaheshimu kazi yake, hivyo kwangu ni kiungo bora kwa hapa nchini," alisema Tshishimbi.

Naye kiungo wa Azam FC, Sure Boy, alisema kwa upande wake anavutiwa zaidi na Chama wa Simba na kueleza idara ya kiungo ya klabu hiyo ya mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam ubora wake unachangiwa na mchezaji huyo raia wa Zambia.

"Kama mtu wa mpira, basi lazima tukubali Simba kwa msimu huu ipo vizuri, hasa ukiangalia safu ya kiungo wamekuwa wakielewana," alisema Sure Boy.

Hadi Ligi Kuu inasimama Simba ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 71 baada ya mechi 28, huku Chama aliyecheka na nyavu mara mbili sawa na Mkude katika jumla ya mabao 63 yaliyofungwa na wachezaji wa timu hiyo hadi sasa, anaongoza kwa kuwa na pasi nyingi za mwisho 'assists' (nane).




Kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na Klabu ya Difaa Hassan El-Jadidi ya Morocco, Simon Msuva, akiogelea nchini humo ikiwa ni sehemu ya kuuweka mwili fiti wakati huu Ligi Kuu ya huko ikiwa imesimama kuepuka kuenea zaidi kwa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19) vinavyoitesa dunia kwa sasa. **PICHA: MAKTABA**

## Katwila kumzuia Kibwana Simba

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kutajwa kuingia katika rada za wachezaji wanaowindwa na Simba, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila amesema hawana mpango wa kumwachia beki wao wa kulia, Shomari Kibwana.

Akizungumza na Nipashe mapema wiki hii, Katwila alisema mchezaji huyo ana mkataba wa muda mrefu na klabu hiyo na bado yupo katika mipango yake.

"Hatuwezi kumuachia Kibwana, bado tunamhitaji kwa kiasi kikubwa kwa sababu ana msaada mkubwa ndani ya timu yetu," kocha na mchezaji huyo wa zamani alisema.

Alisema kwa upande wake hawezi kuruhusu hilo litokee na kwamba kwa sasa hafikirii suala la usajili bali akili yake ni namna ya kuitoa timu hiyo katika nafasi ilipo, na kuiweka katika nafasi nzuri ya kukwepa kushuka daraja.

"Kwa sasa nawaza kuiweka timu yangu nafasi nzuri siwezi kuwaza usajili wakati timu ipo nafasi mbaya," alisema Katwila ambaye timu yake ipo katika nafasi ya 14 baada ya kujikusanyia pointi 33 zilizotokana na kushuka dimbani mara 29.

Katwila alisema lengo kubwa ni kuendelea kushiriki Ligi Kuu kwa kupambana kufa ama kupona.

## Tanzania kushiriki Karate dunia Japan

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Mchezo wa Karate imepata nafasi ya kwenda kushiriki mashindano ya Dunia ya Karate yatakayofanyika nchini Japan Oktoba mwaka huu.

Mashindano hayo ya Karate ya Dunia ambayo hufanyika kila baada ya miaka mitatu, kwa mwaka huu Tanzania imepata nafasi ya kipekee kwa kutoa jaji wa michuano hiyo ambaye ni Sensei Jerome Mhagama.

Mhagama pia ni mkufunzi kuu wa Karate nchini.

Haya yanakuwa mashindano ya 15 ya dunia tangu kuanzishwa kwake, na Tanzania imewahi kushiriki mara mbili tu katika mashindano hayo. Kwa mara ya kwanza ilikuwa mwaka 2011 mashindano hayo yakifanyika nchini Tailand, na Tanzania ilipeleka mchezaji mmoja ambaye alifika katika hatua ya 16-bora.

Mwaka 2014 katika mashindano yaliyofanyika Japan, ushiriki wa Tanzania katika mashindano hayo ilikuwa ni kwa kupeleka jaji pekee.

# Michezo

Ijumaa Machi 27, 2020

Nipashe




## Hazard: Nihukumuni msimu ujao Madrid

HABARI UK 30

HAKUNA KULALA...



Mshambuliaji wa kimataifa wa Ureno na Juventus ya Italia, Cristiano Ronaldo, akidhihirisha kwa upande wake hakuna kulala baada ya jana kuposti picha akiwa gym anafanya mazoezi na ndugu na jamaa zake licha ya wanamichezo wengi kuwapo mapumzikoni kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19). Kutoka kushoto ni Rodrigo Pereira, mpwa wake Alicia, dada yake Katia, Eleanor Caires na dada yake mwingine, Elma. Mchezaji huyo alikwenda Ureno kumjulia hali mama yake aliyepatwa na kiharusi, kabla ya Hispania kutangaza zuio la watu kutoka na kuingia nchini humo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. **PICHA: MTANDAO**

# FRAGA AMTAJA KANDA, KAHATA AKIKATA UTEPE

Abaki akiota mabao yake Coastal, KMC, asema haambiliki kwa makange ya nyama ya mbuzi...

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkata umeme wa Simba, Mbrazil Gerson Fraga, amekuwa mchezaji wa kwanza kukata utepe wa kipindi chao kipya cha mahojiano ya moja kwa moja na mashabiki wao, maarufu kwa jila la "ChatNa" kinachorushwa kupitia mitandao ya kijamii ya klabu hiyo, akianza kwa kuwataja wachezaji wa kikosi hicho wanaompagawisha.

Katika kipindi hicho kilichoanza rasmi jana, Fraga alipoulizwa ni wachezaji gani anawakubali, alisema kuwa wachezaji wa Simba karibuni wote ni wazuri na wana vipaji vya hali ya juu, lakini anaowapenda zaidi ni Francis Kahata, Hassan Dilunga, Meddie Kagere, Miraji Athumani na Deo Kanda.

"Deo Kanda napenda zile chenga zake za maudhi, kama anakwenda huku anarudi," alifafanua.

Hata hivyo, Fraga alieleza kuhuzunishwa na kutokuwapo kwa Miraji kwenye kikosi chao, kwani alikuwa na mchango mkubwa, lakini anachofurahi ni kwamba ameanza mazoezi.

"Namkosa sana Miraji, nilimuuliza lini unakuja, karibu," alisema kwa Kiswahili chake cha kubabaisha.

**Kiungo huyo alibainisha kuwa chakula anachokipenda mno Tanzania ni makange, nyama ya mbuzi na ugali, akidai kuwa akipata chakula hicho na chupa ya maji siku yake inakuwa nzuri mno, tofauti na vyakula vingine.**

Fraga, anayechezea nafasi ya kiungo mkabaji, aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu, alisema mechi yake kubwa anayoikumbuka ya Ligi Kuu ni ile ambayo timu yake ya Simba ilicheza dhidi ya Coastal Union ya Tanga.

Kwenye mechi hiyo Fraga alifunga mabao yote mawili ya ushindi, Simba ikiitandika Coastal 2-0 kwenye Uwanja wa Uhuru Februari Mosi, mwaka huu.

Hata hivyo, amesema bao lake bora ni lile alilolifunga kwenye mechi dhidi ya KMC katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, Desemba 28, mwaka jana alipofunga dakika za nyongeza, Simba ikishinda mabao 2-0, baada ya Kanda kuitanguliza mbele.

"Nililifunga vizuri sana," alisema.

Mpaka sasa Fraga ana mabao matatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ingawa kwa siku za karibuni amekuwa hapati sana nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza.

# Yanga yanywea kimbunga GSM

**Na Saada Akida**

BAADA ya fukuto la kimbunga cha kujiweka pembeni katika majukumu yasiyo ndani ya mkataba wa mdhamini mkuu wa Klabu ya Yanga, Kampuni ya GSM, hatimaye uongozi wa klabu hiyo umekubali yaishi baada ya kuketi meza moja na kuyamaliza kiutu uzima, imefahamika.

Machi 24, mwaka huu Kampuni ya GSM iliuandikia uongozi wa Yanga barua, ikieleza haitafanya jambo lolote ambalo lipo nje ya mkataba kama ilivyofanya ikiwa ni pamoja na kumrudisha kikosini beki, Lamine Moro, kuwasajili Bernard Morisson, Ditram Nchimbi, Haruna Niyonzima na Adeyum Saleh.

**Wadhamini hao pia walieleza kuwa walilipa gharama za kumleta Kocha Mkuu, Luc Eymael na wasaidizi wake, mishahara, usafiri wa ndani, nyumba na tiketi za kwenda na kurudi makwao za makocha hao, huku pia wakilipa mishahara ya wachezaji na bonasi za ushindi katika mechi zote walizoshinda tangu Desemba mwaka jana.**

Lakini juzi kikao kizito kilifanyika na imeelezwa uongozi umeomba radhi kwa tofauti zilizojitokeza na mambo sasa yanakwenda sawa.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alipotafutwa hakupatikana, lakini Ofisa Mhamasishaji wa klabu hiyo, Antonio Nugaz alipoulizwa alisema: "Kila kitu kinaenda vizuri, mashabiki na wanachama wa Yanga watulie, sasa tunaendelea na mchakato wa kuzungumza na wachezaji ambao wanatakiwa kuongezewa mikataba.

"Ni jambo la kumshukuru Mungu hili limepita, mashabiki watulie na kuacha viongozi wafanye yao kuhakikisha tunafanikiwa kile kinachotarajiwa na Wanayanga," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >